# Kongamano ya Huduma ya Vijana Inayomlenga Yesu

barry st. clair

***Huduma ya Vijana Inayomlenga Yesu*** itakusaidia kutimiza ndoto yako ya kibinafsi na ya huduma yako ya vijana kupitia kwa maono yako kufanywa upya, kukupa mpangilio wa mambo yanavyostahili kutazamwa kiuzito huku ikikupa vifaa vya kutendea kazi Kupitia kwa raslimali hii,

Mungu atazalisha maisha yaliyobadilishwa na kuwaandaa wabadilishamaisha kupitia kwako. Hii njia inayotumiwa, na kwa kumlenga Yesu, inakupa kila unachokihitaji kwa maisha na huduma yako. Wewe, mchungaji wako, watu wajitoleao,wazazi na wanafunzi watayaelekea haya maono mamoja yaYesu na hudumaYake ili kukuwezesha:

1. Kuwa na Uhusiano wenye Kina na Kristo
2. Kuomba kwa shauku ili kualika uwepo wa Mungu na nguvu zake.
3. KuwaandaaViongozi kwa huduma yenye kina na itakayodumu.
4. Kuwafuasa wanafunzi kuelekea katika ukomavu ndani ya Kristo
5. Kuipenya Desturi/Utamaduni wa vijana kupitia kwa mahusiano.
6. Kubuni nafasi za kuwafikia wengine kwa ajili ya Kristo.

## Viongozi wa kizazi kichanga …

Kama ndipo unaanza huduma yako, Huduma ya Vijana Inayomlenga Yesu inakupa msingi dhabiti.

Kama tayari unawaandaa viongozi, wazazi na watu waliojitolea, kitabu hiki kinakupa raslimali za kutumia.

Kama wewe unaekeza katika viongozi wengine wa vijana, basi kitabu hiki kitakuwa ni cha kukuongoza kuyaweka katika matendo.

**Huduma yako ya kipekee** itajitokeza unapoyaweka masomo haya katika matendo.
Mtazamo huu wa huduma unaweza kukuweka wewe na kanisa lako katika nafasi ya kukibadilisha kizazi kichanga!



Dr. Barry St. Clair anatamani kukiathiri kizazi kichanga ili kimfuate Yesu. Akiwa mwanzilishi na rais wa Reach Out Youth Solutions, amekuwa katika mstari wa mbele katika huduma ya vijana kwa miaka thalathini akiwahamasisha na kuwaandaa viongozi wa vijana, wazazi, na wanafunzi katika zaidi ya mataifa thalathini. Kupitia kwa uongozi wake, maelfu ya makanisa yameweza kuanzisha mikakati ya huduma ya vijana inayomlenga Yesu. Yeye ni mwandishi wa vitabu zaidi ya ishirini na tano. Barry pamoja na mkewe Lawanna, wana watoto watano walio katika ndoa tayari, wajukuu kumi na wanaishi Atlanta, Georgia.

***Huduma ya Vijana Inayomlenga Yesu*.**

Haki za unakili © 2012 na Huduma ya Reach Out na Barry St. Clair

Kimechapishwa na Reach Out Youth Solutions, www.reach-out.org

Haki zote zimehifadhiwa. Hairuhusiwi kuchapisha, kuiga au kunakili sehemu yoyote ya kitabu hiki kwa jinsi yoyote ile, isipokuwa iwe imeidhinishwa na Huduma Ya Reach Out, Inc.

Kimechapishwa mara ya kwanza, 2002

Mhariri: Barbara L. Townsend

Nakala ya Kiswahili imesanifiwa na Dr. Charles Juma Juma na Mchungaji Joseph Chiteri.

Aya zote za Biblia zimenukuliwa kutoka Biblia ya The Holy Bible, New International Version. Haki ya unakili © 1973, 1978, 1984 na International Bible Society. Zimetumika kwa ruhusa ya Zondervan. Haki zote zimehifadhiwa.

Aya zingine za Biblia zimenukuliwa kutoka kwa Biblia ya THE MESSAGE Haki za unakili © 1993, 1994, 1995, 1996, 2000, 2001, 2002. Zimetumika kwa ruhusa ya NavPress Publishing Group.

Aya zingine za Biblia zimenukuliwa kutoka kwa Biblia ya The Holy Bible: Revised Standard Version. Haki za kunukulu © 1946, 1952, 1971 na kitengo cha Elimu ya Kikristo ya Shirika la Kitaifa la Makanisa ya Marekani (U.S.A.)

# YALIYOMO


UTANGULIZI 5

SEHEMU YA KWANZA: TAZAMA TASWIRA 9

SEHEMU YA PILI: KUWA NA UHUSIANO WENYE KINA NA KRISTO 16

SEHEMU YA TATU: OMBA KWA SHAUKU 32

SEHEMU YA NNE: KUWAANDAA VIONGOZI 43

SEHEMU YA TANO: UANAFUNZI 57

SEHEMU YA SITA: KUIPENYA DESTURI 75

SEHEMU YA SABA: BUNI NAFASI ZA KUWAFIKIA WENGINE 80

KUYAWEKA YOTE PAMOJA 92

MASWALI YANAYOULIZWA KWA WINGI 101

# 'REACH OUT YOUTH SOLUTIONS'

Hutoa mafundisho na vifaa ambavyo husaidia kuwafikia, kuwaandaa na kuwahamasisha vijana kwa Huduma ya Vijana Inayomlenga Yesu kwa ajili ya kila kizazi kichanga kanisani.

***Mchungaji * Mchungaji wa vijana * Wazazi * Mhudumu wa watoto * Watu waliojitolea *Wanafunzi**

## MAONO YETU

Yesu kwa ajili ya kizazi kijacho!

## MWITO WETU

Kuwaandaa na kuwazidisha viongozi
ulimwenguni kote watakaokiathiri kizazi kichanga kumfuata Yesu.

## MBINU YETU

Huduma Ya Vijana Inayomlenga Yesu imetoa
mfumo tofauti kihuduma kwa ajili ya kizazi kichanga itayokuwezesha …

1. Kuwa na Uhusiano wenye Kina na Kristo
2. Kuomba kwa shauku ili kualika uwepo wa Mungu na nguvu zake.
3. Kuwaandaa Viongozi kwa huduma yenye kina na itakayodumu.
4. Kuwafuasa wanafunzi kuelekea katika ukomavu ndani ya Kristo
5. Kuipenya Desturi/Utamaduni wa vijana kupitia kwa mahusiano.
6. Kubuni nafasi za kuwafikia wengine kwa ajili ya Kristo.

## ENEO LETU

**KIMATAIFA.** **'**Huduma ya Reach out Youth Solutions' inaandaa kizazi kichanga katika mataifa zaidi ya thalathini.

**KITAIFA**. Huduma ya 'Reach out Youth Solutions' hutoa mafundisho katika miji, mitaa na vijijini kwa viongozi wa vijana katika kanisa moja na hata katika kongamano za makanisa.

*Kwa habari zaidi kuhusu 'Reach out Youth Solutions' nenda kwa* www.reach-out.org.

# Utangulizi

# Mungu Ana Kusudi na Vijana katika Moyo Wake!

## Na ameliweka kusudio hilo katika moyo wako vilevile!

Kuwafikia vijana, kuwaandaa na kuwahamasisha kwa kusudi la Mungu ndilo jambo la muhimu sana katika kanisa la karne hii.

Lakini sasa tufanye nini ili tulitimize kusudio hilo katika njia itakayoiangazia huduma yake Yesu Kristo kama mfano na msingi?

Kupitia *Huduma ya Vijana Inayomlenga Yesu*!

Kwa maana mtu hawezi kuuweka msingi mwingine ila uliowekwa tayari nao ni Yesu Kristo.

1 Wakorintho 3:11

Watu walikuwa wakimletea Yesu watoto wadogo ili awaguse lakini wanafunzi wake wakawakemea. Yesu alipoona yaliyokuwa yakitukia alichukizwa, akawaambia wanafunzi wake, "waacheni watoto wadogo waje kwangu, wala msiwazuie, kwa maana Ufalme wa Mungu ni wa watu kama hawa. Amin, amin nawaambia, mtu ye yote asiyekubali Ufalme wa Mungu kama mtoto mdogo, hataingia kamwe." Akawachukua watoto mikononi mwake, akawakumbatia akaweka mikono yake juu yao akawabariki.

Marko 10:13-16.

# Jinsi Ya Kufaidika Zaidi

Kama ukikamilisha *Huduma ya Vijana Inayomlenga Yesu*, tumaini letu ni kwamba huduma yako itabadilika na kuwa ya kipekee. Tamanio letu si kwamba huduma zote zitakazohusiana na *Huduma ya Vijana Inayomlenga Yesu* zifanane nayo. Ndoto yetu ni kinyume na hayo. Badala yake, twatumaini kwamba huduma yako ina mguzo wa kipekee wa Mungu unaoifanya kuwa tofauti na huduma zingine zote. Kwanini? Ni njia ya kipekee ya Mungu kujieleza kupitia kwako na kanisani.

*Huduma ya Vijana Inayomlenga Yesu* inakupa "taswira kuu" ya mtazamo ambavyo Yesu alivyoifanya huduma na vile unavyoweza kumuiga katika huduma yako. Kwa hali, ni kizuu ambacho utakitia nyama. Ni nyumba utakayoipamba. Huduma hii ya vijana inayomlenga Yesu inakupa msingi ambao waweza kuujengea huduma yako yote.

Kama hujawahi kutumia vitabu vyetu ama hauna ufahamu wowote juu ya mkakati huu, basi huu ni utangulizi. Utapata yote unayohitaji ili uweze kuanza.

Kama umetumia vitabu vyetu hapo awali ama umehusika katika mafundisho yetu ya aina yo yote, basi huu ni wakati wa kutekeleza. Itakusaidia kujipanga kulingana na umuhimu wa mambo, kuthibitisha kazi yako na kuiboresha huduma yako.

Ukichukua changamoto ya kuandaa viongozi wa vijana, tumia kitabu hiki wakati wa kufundisha.

## Jinsi ya Kujifunza Mafundisho Haya

1. Kwa kutumia mpango kiratiba, weka ratiba ya sehemu nane, kila moja ikichukua muda wa saa moja. Unaweza kupangia wakati huu mara moja kwa juma au mara moja kwa siku, au kama inawezekana unaweza kuchukua muda wa siku mbili au tatu mfululuzo. Kwa uaminifu hakikisha umetimiza ahadi yako.
2. Katika wakati huu, hakikisha umezima simu yako. Usimruhusu mtu akusumbue. Kimaombi, tumia mwongozo wa kujadiliana ili ukusaidie kuandika muhtasari. Msikize Mungu anavyokuelekeza. Andika muhtasari na kunakili mawazo kimaombi. Usiwe na haraka.
3. Kwenye tuvuti ya www.reach-out.org, shusha CD zinazopatikana bure kisha uzisikize mara nyingi.

4. Chukua hatua zinazostahili ukitumia mkakati wa utendaji. Kifaa hiki hakijabuniwa kama zoezi la akili. Bali hutoa maoni na hatua za hakika za kufuatilia maono hayo.
5. Tenda mara moja mambo yanayojitokeza na unaamini kuwa ni ya dharura.

## Jinsi ya Kutumia Mafundisho Haya na Watu Wajitoleao

Unapojihusisha na *Huduma ya Vijana Inayomlenga Yesu*, utaweza kutambua kwa haraka, kitu muhimu zaidi katika huduma ya vijana ni kuunda kundi la viongozi. Unaweza kutumia mafundisho haya kwa urahisi kubuni maono na mwelekeo katika maisha ya watu waliojitolea.

Unaweza kutumia mafundisho haya wakati wa faragha ama katika vipindi kadhaa kutoa maono yako kwa watu waliojitolea au kuwahimiza kutumia "taswira" ya huduma ya vijana. Ili kuwasilisha mafundisho haya kwa watu waliojitolea, fikiria mambo yafuatayo:

1. Jifahamishe na mafundisho ya kitabu hiki. Fanya muhtasari kutoka kwa mafundisho yaliyoko katika kitabu hiki, ongezea hadithi zako mwenyewe na mifano.
2. Amua mahali pa kukutanikia. Ikiwezekana, panga mkutane nyumbani kwako au katika nyumba ya mmoja wa wana kundi. Kukutanika sebuleni au mezani kwa kinywaji kutasaidia watu kuwa huru kutoa maoni yao na kujadiliana katika kundi.
3. Panga muda wa kukutanika. Kila kipindi chaweza kuchukua muda wa saa moja au moja na nusu. Dakika 15 za kuomba, kufanya marudio na kushiriki, dakika 45 za mafundisho na majadiliano, na dakika 15 za kuwaombea wanafunzi.
4. Wape vitabu. Waweza kununua nakala zaidi za *Huduma ya Vijana Inayomlenga Yesu* kwa ajili ya kundi lako, au waweza kuulizia nakala za kitabu hiki na vingine kupitia tuvuti ya www.reach-out.org.
5. Jiandae sawasawa. Anza maandalizi ya kuongoza kipindi hiki mapema.

6. Anza bila kuchelewa. Heshimu ahadi ambazo viongozi wako wamefanya.
7. Hakikisha mazungumzo yenu yako ndani ya mafundisho. Uliza maswali kwa udhahiri na kwa ufupi. Heshimu maoni ya kila mmoja. Dumu katika Maandiko, usikubali kutoka nje ya Maandiko. Tia changamoto kwa majibu ya kawaida au ya juu juu. Uliza maswali ya marudio. Hakikisha kila mmoja amehusika.
8. Tia mkazo jinsi mafundisho haya yanavyoweza kutumika. Baada ya kila kipindi, wape muda waweze kufikiria na kuandika "hatua za kuchukua." Wape muda wa kujadiliana yale wameyaandika. Waulize waweze kuamua hatua moja watakayoichukua juma hili. Wachagulie wenzi watakaokuwa na jukumu la kuwatia moyo kutenda walivyokusudia.

## OMBI LANGU KWAKO

'Nazidi kumuomba Mungu wa Bwana wetu Yesu Kristo, Baba wa utukufu, awajalieni roho ya hekima na mafunuo mpate kumfahamu zaidi. Ninaomba pia kwamba macho ya mioyo yenu yaangaziwe ili mpate kujua tumaini mliloitiwa na mtambue utajiri wa urithi wa utukufu wake kwa watu wa Mungu, na muufahamu uweza wake usiopimika ambao ametupa sisi tunaoamini"

Waefeso 1: 17-19[a]

# Tazama Taswira Kuu

## Lengo

Kuyashika maono ya
Huduma ya Vijana Inayomlenga Yesu

Sehemu ya kwanza

Tazama Taswira Kuu

1

# KUMTAZAMA YESU

Tukichambua Injili, tutaona kuwa Yesu alifuata huduma yenye mtindo wa elimumwendo. Aliieleza baada ya Mafarisayo kumshitaki kwa kuponya siku ya Sabato na baada ya kudai kuwa sawa na Mungu.

> Yesu akawaambia, Amin amin nawaambia, Mwana hawezi kufanya jambo lo lote peke yake, Yeye aweza tu kufanya lile analomwona Baba yake akifanya, kwa maana lo lote afanyalo Baba, Mwana pia hufanya vivyo hivyo.
>
> Yohana 5:19

Kwa kuwa karibu na Baba yake, Yesu alipata maagizo kutoka kwa Baba yake na kuyafuata. Hiyo iliyafanya yale aliyoyatenda kila siku kuwa si tu elimumwendo, bali ya kipekee. Jambo moja tunaloweza kusema juu ya huduma zetu ni kuwa: Mungu anataka ziwe elimumwendo za kipekee, zikiwa na msingi thabiti katika uhusiano wa kindani sisi naye. Kusudi la kujifunza namna ya kujiandaa katika *Huduma ya Vijana Inayomlenga Yesu* si kuanzisha huduma inayofanana na huduma za watu wengine, bali kuanzisha huduma ya elimumwendo na ya kipekee, iliyo na hisia kali ya kumfuata Yesu. Hayo hutoka ndani ya moyo unaotamani kuona yale Mungu anayoyatenda na baadaye kuyatenda.

Yesu alimtazama Baba yake. Nasi, tumtazame Yesu. Tunapomtazama Yesu, je, huwa tunaona nini? Huwa tunaona mwenendo Yesu alioufuata katika matendo yake. Tunagundua kanuni ambazo Yesu alifuata na hutupa mwelekeo wa kuendeleza huduma zetu. Kanuni zisizongumu au ghibu, bila kumwekea Mungu mipaka, hata hivyo Yesu alikuwa na mkakati. Je, ulikuwa wa namna gani?

***Jesu alimtii Baba yake***. Tukio la Yesu alipokuwa akiumia vibaya katika shamba la Gethsemane huonyesha wazi utiifu wa Yesu kwa Baba yake. Tukio hili la Yesu hututia changamoto ya kutii.

***Yesu aliekeza maisha yake katika wanafunzi wake***. Tukitazama kwa mbali twaweza kuona mambo ambayo Yesu aliwakabidhi wanafunzi wake. Kwa miaka zaidi ya mitatu, walipitia mafundisho makali sana ya uongozi. Aliwaongoza kujitolea na kujazwa na Roho wake Mtakatifu. Alienda nao wakati wa huduma zake na akawasaidia walipokuwa wakihudumu. Kwa kufanya hivyo, aliwaongoza kuhubiri Habari Njema, kuponya waliovunjika moyo na kuwaweka huru watumwa. Aliwapa nguvu kuendeleza huduma waliyokuwa wameiona ndani yake kwa njia yao ya kipekee. Kutokana na hayo aliandaa kundi la viongozi ambalo lilibadilisha ulimwengu.

***Wanafunzi wa Yesu pia waliekeza maisha yao katika wengine***. Kuendelea kuwakabidhi wengine Kwa njia ya uanafunzi ndilo lililokuwa lengo la huduma yake Yesu, vivyo hivyo, la kanisa la kwanza. Watu waliendelea kutoa maisha yao kwa wengine, kwa ajili ya ufalme wa Mungu. Hiyo ilisongeza kanisa mbele kama chombo kilichobadilisha watu waliokuwa karibu nao na baadaye kubadilisha ulimwengu. Kukabidhi kundi dogo la "wanafunzi wa Yesu" kuwafundisha kuwa "watumwa wa Yesu" ndiyo huduma njema kuliko zote. Na ikifanywa kama vile Yesu alivyoifanya, kuwafundisha wengine haitabadilisha wale tu wanaofundishwa bali, kwa muda, itabadilisha ulimwengu wote.

Kubadilisha ulimwengu kupitia Habari Njema ya Injili ilichukua nafasi ya kwanza katika maisha ya wanafunzi katika kanisa la kwanza kwa sababu waliona jinsi ilivyokuwa muhimu kwa Yesu. Alitoa vizuizi vyote na kuleta usawa kwa kutengamana na wote; malaya, viwete, maskini na vipofu. Kwetu sisi, kama Yesu, kuwafundisha wengine wakati mwingi huwafanya wengine kukua katika maisha yao ya kiroho, na baadaye kuelekea katika huduma nje ya kuta za kanisa.

Katika maisha ya Yesu, huduma yake iliwavutia watu wengi. Kufundisha, kuponya, kuhubiri, kutoa mapepo, kulisha watu elfu tano kwa mikate mitano na samaki wawili. Haikujalisha yale aliyofanya. Yesu aliwavutia wengi! Haikuwa juu ya wanafunzi au jinsi ya kuwafanya watu kuwa wanafunzi. Haikuwa juu ya miujiza ya ajabu aliyofanya, au mafundisho ya kindani aliyofundisha au jambo lingine lo lote. Ilikuwa juu ya Yesu! Yeye alikuwa yu nani na kile alichokuja kufanya ndicho kilikuwa kiini. Hii ndiyo tunayohitaji katika kanisa – *Huduma ya Vijana Inayomlenga Yesu*. Huduma nyingine yoyote itatuwacha bila cho chote na haitaweza kutukamilisha. Kama Yesu, tunataka tuwache alama ya milele ambayo haitafutwa - basi tumfanye Yesu kuwa lengo letu.

## MASWALI MAGUMU

Kutazama mahali tulipo kwa uaminifu si jambo rahisi kwa wengi wetu. Lakini kujua mahali tulipo ndiyo njia ya pekee ya kufikia mahali tunapotarajia. Kwa hivyo, jiulize haya maswali magumu ili uweze kuona kama mtazamo wako uko kwa Yesu. Jibu maswali haya kwa kiwango cha 1 hadi 10: 1 ni kiwango cha chini kabisa, na 10 ni kiwango cha juu kabisa.

1. Unakadiria vipi muda wako na mawazo yako unayoyaelekeza katika kutafuta uhusiano wa kina naye Bwana Yesu?

   1 2 3 4 5 6 7 8 9 10

2. Kwa kiwango kipi watu wako waliojitolea, wazazi, na wanafunzi wametenga mahali na wakati wa kuombeana na kuwaombea vijana wanaomhitaji Yesu?

   1 2 3 4 5 6 7 8 9 10

3. Je, watu wako waliojitolea wamejitolea vipi kwake Yesu, mmoja kwa mwingine, na kwa huduma yoyote yenye uhusiano na au ya wanafunzi/vijana?

   1 2 3 4 5 6 7 8 9 10

4. Asilimia ngapi ya waamini katika huduma yako wanajihusisha kindani na kikundi cha uanafunzi kinachoendelea?

   1 2 3 4 5 6 7 8 9 10

5. Ni asilimia ngapi ya watu wako waliojitolea wanajiona kuwa ni wa ushawishi mkubwa kwa wanafunzi na vijana kwa ajili ya Kristo?

   1 2 3 4 5 6 7 8 9 10

6. Ni asilimia ngapi ya idadi yote ya wanafunzi uliowafikia mara ya mwisho walikuwa hawajamtambua Mungu kuwa mwokozi wao?

   1 2 3 4 5 6 7 8 9 10

*Kujibu kwako maswali haya yote kwa uaminifu kutakufanya uweze kutazama huduma yako mara tena kwa kumaanisha. Tumaini hapa ni kuwa maswali haya yatakupa tamaa ya kubadilika. Katika kila sehemu itakayofuatia, utapata nafasi ya kutafakari zaidi unapojibu maswali , yatakayoambatana na sehemu hizo.*

# KANUNI ZA HUDUMA YA VIJANA

**Tutawezaje kupata maono ya huduma ya vijana inayomlenga Yesu?**

## Gundua Maono

Soma Mathayo 9:35-38 mara sita. Katika kifungu hiki utapata vidokezo vya huduma ya vijana inayomlenga Yesu! Kila wakati muulize Mungu akusaidie kutambua jambo moja.

> *"Yesu alitembelea miji yote na vijiji, akafundisha katika masinagogi yao akihubiri Habari Njema ya ufalme wa Mungu, na kuponya magonjwa yote na udhaifu wa kila namna. Basi, alipowaona watu, makundi kwa makundi, aliwaonea huruma kwa sababu walikuwa hoi na wenye wasiwasi kama kondoo wasio na wachungaji. Hapo akawaambia wanafunzi wake, `mavuno ni mengi, lakini wafanyakazi ni wachache. Basi mwombeni Bwana wa mavuno awatume wafanya kazi kwenye mavuno yake'"*
>
> ***Mathayo 9:35-38.***

Katika aya ya 35-36, unaona vielekezi vipi kuhusu jinsi Yesu alivyowazia na kuwashughulikia watu?

Yesu aliwapa wanafunzi wake vielekezi vipi kuhusu maono yake alipowashauri katika aya za 37-38?

Kuzisoma haraka au kuzipitia injili zote nne zitakupa mambo muhimu katika kuishi kwake Kristo. Soma Mariko 1-4, au Injili zote na utapata kwamba zote zinaelezea wepesi wa maisha na huduma yake Yesu. Kurasa zote zinamlenga Yesu!

## Eleza Kizazi Kichanga

Kulingana na Mathayo 9:35-38, Yesu aliuelezaji umati uliokuwa mbele yake? Maelezo hayo yanawafanana vipi vijana unaowajua?
Fasili kila neno na ueleze jinsi linavyokifana kizazi kichanga.

Hoi

Wenye wasiwasi

Kondoo wasio na wachungaji

Utafiti unaonyesha kuwa Yesu alikuwa anakieleza kizazi kichanga katika maelezo hayo yake.

---

## KILA MASAA 24. . . (Marekani)

Wanafunzi 17,297 hutimuliwa kwa muda kutoka shuleni.

Taarifa hutolewa juu ya wanafunzi 7883 kudhulumiwa, au kutotunzwa.

Wanafunzi 248 hutiwa mbaroni

Wanafunzi 2861 huacha shule

Wanafunzi 1329 hupata watoto wakiwa bado wachanga sana

Wanafunzi 367 hukamatwa kwa kutumia madawa ya kulevya.

Wanafunzi 180 hukamatwa kwa kuhusika katika uhalifu wa mabavu.

Wanafunzi 180 huhusika katika mauaji ya wanadamu

Wanafunzi 5 hujiua wenyewe

Mwanafunzi 1 hufa kwa sababu ya UKIMWI

**Haya ni kulingana na kikokoto cha siku moja ya shule (siku 180, masaa saba kwa siku) © 2002 Children's Defense Fund.)**

---

Tafuta neno ambalo Yesu alilitumia katika Mathayo 9 : 36 kuelezea hisia zake kuhusu watu waliomzingira.

Andika jina la mwanafunzi au kijana mmoja unayemjua anayechukua taswira/picha ya maelezo ya Yesu kuhusu kizazi kitakachofuata:

______________________________________________

Toa maelezo kumhusu kijana huyo kulingana na hali yake ya maisha, fikra, tabia, uchaguzi na matendo.

Je, unahisi kumhusu kijana huyo jinsi Yesu alivyohisi kuhusu watu waliomzingira?

Andika ombi lako kwake Mungu kwa mwanafunzi huyo.

Tumia yale yote unajifunza katika Huduma ya Vijana Inayomlenga Yesu ili uweze kumfikia mwanafunzi au kijana huyo na wengine kama yeye.


## Ona jinsi Unavyoweza kuleta mabadiliko

Chunguza kwa makini Mathayo 9:38

Katika kifungu hiki, Yesu anatoa mkakati unaoleta mabadiliko katika maisha ya watu walio "hoi , wenye wasiwasi kama kondoo wasio na mchungaji." Tazama urahisi wa mkakati huu.

| **Yesu: "Basi mwombeni Bwana mwenye mavuno . . . awatume wafanya kazi . . . wavune mavuno yake."** | | | |
|---|---|---|---|
| **KITENDO** | **OMBA**<br>Kumtafuta Yesu | **ANDAA**<br>Kuzidisha idadi ya viongozi | **FUNDISHA INJILI**<br>Kuwafikia watu |
| **MKAKATI** | -Kuwa na uhusiano wenye kina na Yesu<br><br>-Omba kwa shauku | -Andaa Viongozi<br><br>-Uanafunzi | -Kuipenya desturi<br><br>-Buni nafasi za kuwafikia wengine. |

# Tazama Taswira Kuu




Tukiwa na taswira katika akili zetu, twaweza kuona jinsi ya kuunda huduma ya vijana katika kanisa letu na pia jinsi ilivyo rahisi kumfikia kila mwanafunzi katika kila shule na ujumbe wa Yesu kristo wa kubadilisha maisha.

# Itafakari Taswira Kuu

Mkakati huu unaomlenga Yesu ulio katika Mathayo 9:38 unayaandaa mazingira ya kuomba kwa shauku na baadaye huongezea polepole juu ya *kanuni tano muhimu* katika mazingira ya kuandaa na kufundisha Injili. (Tazama taswira katika ukurasa wa 17).

## Kuwa na Uhusiano Wenye Kina na Kristo

Ni kwa njia gani unaweza kuwa na uhusiano na Yesu? ***Kuwa na uhusiano wa karibu na wa kindani na Yesu na kuishi katika uhusiano huo kwa kumtumikia Kristo na kudhihirisha tabia yake kwa wale walio karibu nawe*** (Marko 1:7-8).

## Kuomba Kwa Shauku

Utaombaje ili upate kuuvuta uwepo wa Mungu katika huduma yako? ***Unda mkakati wa maombi unaokuhusu wewe, watu waliojitolea, wazazi na wanafunzi.*** (Mathayo 18: 18-20)

## Kuwaandaa Viongozi

Je, wawezaje kuwaandaa viongozi wenye sifa ya kuwa na huduma ya kina na ya muda mrefu? ***Andaa viongozi walio na moyo na ustadi wa kuwafikia na kufanya uanafunzi*** (Mark1:16-20).

## Uanafunzi

Je, huwa unafanya uanafunzi kwa njia gani ili vijana wawe na shauku ya kiroho na waweze kuvutia marafiki zao kiroho? ***Patia vijana changamoto ya kukua kiroho katika uhusiano wao na Yesu kupitia kwa kundi ndogo la uanafunzi*** (Marko 3:13-15).

## Kuipenya Desturi

Wawezaje kuwapa motisha na kuwahamasisha viongozi na wanafunzi kuingia ndani ya desturi za wanafunzi? ***Enda mahali wanafunzi/vijana walipo na ujihusishe na mambo yao na kuwaandaa kuwafikia marafiki zao katika desturi zao.*** (Marko 1:40-42).

## Buni Na fasi za Kuwafikia Wengine

Unawezaje kubuni nafasi za wanafunzi kuwafikia marafiki zao?

***Panga kipindi kinachowafaa wanafunzi ambapo wanafunzi wataweza kuwaleta wanafunzi wengine wasiowaamini, ili waweze kuwa na wakati wa kusikia habari hii ya Yesu ya kubadilisha maisha yao*** (Marko 4:1-2).

# HATUA ZA KIUTENDAJI

Ukiwa na taswira ya Huduma ya Vijana Inayomlenga Yesu inamaanisha kuwa umeelewa wazo hilo.

Tumia hatua hizi za utendaji ili uweze kupata maono yako:

- Kariri Mathayo 9:35-38. Kariri tena na tena mpaka ujisikie ni kama i sehemu yako.
- Chukua picha ya mwanafunzi au kijana ambaye jina lake uliandika kama "hoi, mwenye wasiwasi kama kondoo wasio na mchungaji." Weka picha hiyo katika Biblia yako ili ikukumbushe juu ya watu unaokusudia kuwafikia
- Amua shughuli au huduma zinazofaa mkakati wa Huduma ya Vijana Inayomlenga Yesu na mahali panapostahili. Kuwa wazi kwa zile shughuli ambazo hazifai.

Sehemu ya pili hadi ya saba zitachunguza kwa undani kila mtazamo wa huduma ya vijana inayomlenya Yesu na itakuongoza kuyaona maono yake Yesu kwa huduma yako wazi kabisa.

| **Shughuli za Sasa au Huduma** | **Omba** | | **Andaa** | | **kuwafikia** | | **HAIKUBALIKI** |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Kuwa na uhusiano wa karibu na Kristo | Kuomba kwa shauku | Kuwaandaa viongozi | Kuwafuasa wanafunzi | Kuipenya desturi | Kubuni nafasi za kuwafikia wengine | |
| | | | | | | | |

# Kuwa na Uhusiano wa Kina na Kristo

## Lengo

Kufuatilia Kuwa na Uhusiano
Wa Kina na Kristo

Sehemu ya Pili

# KUMTAZAMA YESU

Baba, Mwana na Roho Mtakatifu wanatuita tuenee katika Kristo.

**Mungu Baba**. “Hapo mwanzo, Mungu. . .” Biblia huanza. Kabla ya wakati, Mungu alikuweko! Wakati ulipoanza, Aliumba kila kitu – “mbingu na dunia” (Mwanzo 1:1). Kutoka uumbaji, Mungu yupo, sasa, wakati huu, Mtawala wa vitu vyote. Mwandishi wa Zaburi aliieleza hivi: “Mwenyezi Mungu ameweka kiti chake cha enzi mbinguni; yeye anatawala juu ya vitu vyote” (Zaburi 103:19). Wazo hili limerudiwa katika Biblia yote. Kwa mfano, Paulo katika Waefeso 4:6 aliandika kuwa “Kuna Mungu mmoja na Baba wa wote, afanya kazi katika yote na yuko katika yote.” Hata hivyo Biblia husema kuwa **Mungu atakuwa**. Hapo mwisho ataendelea kutawala. Mtume Yohana aliandika juu yake, “Nikasikia viumbe vyote mbinguni, duniani, chini ya dunia na baharini – viumbe vyote ulimwenguni – vikisema: `Kwake yeye aketiye katika kiti cha enzi, na kwa Mwanakondoo, iwe sifa na heshima na utukufu na enzi, milele na milele!’” (Ufunuo 5:13.) Mungu hutawala uumbaji wake na viumbe vyake.

**Mungu Mwana**. Mungu Baba alimpa Yesu mamlaka yake yote. “Nimepewa mamlaka yote mbinguni na duniani . . .” Yesu akawaambia (Matthew 28:18). Mtume Paulo, mara kwa mara alieleza mamlaka ya Yesu ya mwisho. Katika Waefeso 1:19-22, Paulo anaeleza uwezo wa Yesu.

*Mpate kutambua jinsi uwezo wake ulivyo mkuu mno kwa ajili yetu sisi tunaoamini. Uwezo huo unaofanya kazi ndani yetu ni sawa na nguvu ile kuu mno aliyomfufua nayo Kristo kutoka wafu, akamketisha upande wake wa kulia wa mbinguni. Huko, Kristo anatawala juu ya kila tawala, mamlaka, enzi na ukuu; anatawala juu ya kila cheo kiwezacho kutajwa katika ulimwengu huu na katika ulimwengu ujao. Mungu ameweka vitu vyote chini ya miguu yake, akamkabidhi kwa kanisa akiwa mkuu wa vitu vyote . . .* *Waefeso 1:19-22*

Akifafanua Yesu yu nani, mwandishi wa Waebrania alieleza Mwana katika Waebrania 1:3 kama

- Mrithi - Baba yake alimchagua kuwa “Mrithi wa vyote”
- Muumbaji – Mungu, kupitia  kwa Yesu, “Aliuumba ulimwengu.”
- Mng’ao – Yesu ni “mng’ao wa utukufu wa Mungu.” Yesu ni “mfano kamili wa hali ya Mungu mwenyewe.”
- Mtegemezi – Kila sekunde, kila mfumo umewekwa pamoja “kwa neno lake lenye nguvu.”
- Mtakasi – Kwa kujitolea kufa msalabani, Yesu, aliwatakasa binadamu dhambi zao.”
- Mtawala – Baada ya ufufuo, Yesu “ameketi huko juu mbinguni, upande wa kulia  wa Mungu mkuu” ambako hutawala na kujidhihirisha.

Bila shaka Yesu ni Bwana! Na siku moja,

> “kila goti litapigwa na kila ulimi utakiri kwamba Yesu Kristo ni Bwana, kwa utukufu wa Mungu Baba.”
>
> *Wafilipi 2:10-11.*

**Mungu Roho Mtakatifu**. Naye Mwana akamkaribisha Roho Mtakatifu kuishi ndani yetu ili tuweze kuelewa Mungu yu nani, yale Yesu ametutendea na jinsi ya kuishi katika uwepo wa Roho Mtakatifu. Mtume Paulo hutuambia: kwa vile sasa nyinyi ni wanawe, Mungu amemtuma Roho wa Mwanawe mioyoni mwenu, Roho ambaye hulia “Aba,” yaani “Baba” (Wagalatia 4:6).  Na kwa sababu sisi ni wana, sisi si watumwa wa dhambi tena. “Bali Mungu amekufanya pia mrithi” (Wagalatia 4:7). Kwa sababu Roho Mtakatifu huishi ndani yetu, yeye hutupa nguvu na uwezo wa kuelea na kuendelea katika Kristo, nguvu za kuishi jinsi anavyotaka, na agano la maisha yetu ya milele. Kwa sababu hayo ni kweli, Mtume Paulo anatupa changamoto, “Basi nasema hivi: mwenendo wenu na uongozwe na Roho, nanyi hamtafuata tena tamaa za kidunia . . .Tukiishi kwa msaada wa Roho, na tufuate mwongozo wake” (Wagalatia 5:16, 25).

Twaweza kufikia uamuzi kuwa Baba, Mwana na Roho Mtakatifu hutawala ulimwengu mzima na hiyo ni pamoja nasi. Kwa sababu sisi ni wana wa Mungu, kwa kuwa tumekuwa na uhusiano wa karibu naye, tumechagua kuishi chini ya utawala na uongozi wa Mungu – Ubwana wa Kristo. Kwa kila maamuzi yetu ya kila siku, tunatambua kwamba, “Wewe ni Mungu, na mimi si Mungu!” Tuna hamu ya kutoa mawazo yetu, mtazamo na matendo yetu kwa Kristo.

**Kwa Neema ya Mungu.** Kumfanya Yesu kuwa Bwana katika maisha yetu ina maana kuwa anaendelea kuwa na uhusiano wa karibu na wa kibinafsi nasi. Ili tuweze kutambua nafasi yetu katika uhusiano huo, na tuwe na uhusiano wa karibu na Kristo, ni lazima tuyafanye yale anayoyataka. Tunapompa matumaini yetu, temegeo, ndoto na uamuzi kila siku basi twaweza kuishi mbele zake kila wakati, tukimfurahia!

Mtume Paulo alitoa taswira halisi ya jinsi ilivyo kuishi chini ya uongozi wa Yesu Kristo. Paulo alikuwa na "maumivu mwilini kama mwiba." Sisi sote huwa nayo. Mwiba huo ulikuwa wa Paulo lakini kwetu sisi ni mambo kama udhaifu wa kimwili, matatizo katika uhusiano wetu, kupoteza mpendwa, tabia za dhambi. Twaweza kujaza katika pengo. Mungu alitumia "Maumivu mwilini kama mwiba" kumfanya avunjike. Mungu anataka tuvunjike. Ni katika kuvunjika kwetu ndipo tutamfanya Yesu kuwa Bwana wa maisha yetu. Paulo alimwomba Mungu amuondolee mwiba. Hakufanya hivyo! Lakini akamwambia, "Neema yangu yatosha kwa ajili yako; maana uwezo wangu hukamilishwa zaidi katika udhaifu" (2 Wakorintho 12:9). Hatuishi maisha ya Kikristo kwa uwezo wetu. Lakini twaishi kwa neema ya Mungu – uwezo wake wa ajabu ndani yetu kupitia kwa msalaba na ufufuo. Katika kuvunjika kwetu twajifunza kuishi kwa neema ya Mungu. Neema yake huachilia nguvu zake kwetu. Basi kama Paulo, twaweza kusema,

> "Basi, ni radhi kabisa kujivunia udhaifu wangu ili uwezo wake Kristo ukae juu yangu. Kwa hiyo nakubali kwa radhi udhaifu, dharau, taabu, udhalimu na mateso, kwa ajili ya Kristo; maana ninapokuwa dhaifu, ndipo ninapokuwa na nguvu"
>
> 2 Wakorintho 12:9-10

Katika kuvunjika kwetu tunakuwa katika uwepo na nguvu za Mungu.

> *'Ee Mungu, nimejaribu wema wako, na umeniridhisha na umenitia kiu. Najua nahitaji neema yako. Nina aibu kubwa kwa kukosa kukutamani. Ee Mungu, uliye na nafsi tatu katika moja, nataka kukutaka, nataka kujazwa na kukutamani, nina kiu cha kufanywa kuwa na kiu'* A.W. Tozer

**Mwaliko kwa uhusiano wa Kina**. Mungu ambaye anatawala na kuongoza ulimwengu anatupenda na kupendezwa nasi. Hata sasa anaendelea kutufuata kwa upendo mwingi. Kwa njia ya Kristo ametutengenezea njia tuweze kumfuata. Ametupa kila kitu tunachohitaji ili tuweze kumjua na kumpenda. Anatuita ili, "Umpende Bwana Mungu wako kwa moyo wako wote, kwa roho yako yote na kwa akili yako yote" (Mathayo 22:37). Kila siku anatuita ili tuingie katika uhusiano wa karibu naye, na chini ya mamlaka ya Yesu, tumfuate kwa upendo. Kila siku, tunapoendelea kutamani kuwa na mizizi imara katika Kristo, hapo ndipo tutajua kwamba Yesu ni Bwana.

---

## Ombi La Kujiachilia

*Baba, najiachilia mikononi mwako;*

*nitende upendavyo.*

*Lolote ulitendalo, nakushukuru.*

*Ni tayari kwa yote,*

*nakubali yote.*

*Naiachilia nafsi yangu mikononi mwako;*

*nakupatia na upendo wa moyo wangu wote,*

*kwani nakupenda Bwana,*

*na hivyo kujisalimisha kwangu*

*pasipo na kizuizi chochote na kwa ujasiri wote,*

*kwani wewe ndiwe Baba yangu.*

*Amen!*

*Charles de Foucauld*

---

## MASWALI MAGUMU

Tafakari maswali haya. Jiweke katika kiwango cha 1-10. Angalia jinsi umejibu maswali hayo. Andika aya fupi ukieleza kwa ukweli, uamuzi ambao unahitaji kuchukua kuhusu shauku yako kwake Yesu.

1. Jipe kiwango cha shauku yako kwa Mungu?

   1 2 3 4 5 6 7 8 9 10

2. Utalinganisha vipi shauku ya Mungu kwako?

   1 2 3 4 5 6 7 8 9 10

3. Kwa kweli, unafikiria Mungu anakupenda kiasi gani, hata kwa yale yote anayoyajua kukuhusu?

   1 2 3 4 5 6 7 8 9 10

4. Uhusiano wako na Mungu wa karibu ni wa kiwango gani?

   1 2 3 4 5 6 7 8 9 10

5. Wewe, u msafi kiasi gani katika akili, roho, maisha na uhusiano wako?

   1 2 3 4 5 6 7 8 9 10

6. Je, wewe u mtakatifu kiasi kipi?

   1 2 3 4 5 6 7 8 9 10

Uamuzi wangu wa uaminifu kuhusu ubwana wa Yesu maishani mwangu

# KANUNI ZA HUDUMA YA VIJANA

**Unawezaje kuendelea na uhusiano wa karibu na Yesu ambao unakuelekeza kumpenda Yesu zaidi?**

## Lengo: Upendo

Soma 1 Timotheo 1:5 mara tatu. Andika muhtasari na uongeze utambulizi mpya kutoka kwa kifungu kila wakati unapokisoma. Kifungu hiki kina mambo ya utendaji ambayo yatatusaidia kuunda njia ya kumfuata Yesu kwa upendo.

> *Shabaha ya amri hii ni kuhimiza upendo utokao katika moyo safi, dhamiri njema, na imani ya kweli*
>
> *(1 Timotheo 1:5).*

**Upendo hutokana na . . .**

- Moyo safi

- Dhamiri njema

- Imani ya kweli

# Kuelekea uhusiano wa kina na Yesu

Jipe changa moto kwa kuzingatia maswali haya huku ukitafakari kuhusu maandiko ili kuelekea katika uhusiano wa kina na Yesu.

Unapojibu maswali haya saba muhimu na utende kulingana nayo yatakufungulia njia ya kuwa na uhusiano na Yesu.

## Moyo Safi

1. Je, nina mawazo maovu kuhusu watu wa jinsia tofauti? (2 Timotheo 2:22)

2. Je, mimi hulalamika, kunung'unika au kuwa na nia mbaya? (Wafilipi 2:14-15).

## Dhamiri Njema

3. Je, mimi huwatii na kuwaheshimu wazazi na jamii yangu? (Waefeso 6:1-4).

4. Je, machungu ya moyo na kutotii kunanizuia kuwasamehe wengine? (Mathayo 6:14-15).

5. Je, nimemtendea mtu mwingine vibaya? (Mathayo 5:23-24).

## Imani ya Kweli

6. Je, mimi husema uongo, huiba au hudanganya? (Wakolosai 3:9).

7. Je, kunayo sehemu yoyote maishani mwangu ambapo sijampa Yesu kipaumbele? (Mathayo 6:33).

# HATUA ZA UTENDAJI

Leo hii, chukuwa dakika kumi na tano za kutafakari na uandike chini mambo yampendezayo Mungu kukuhusu.

- Kutokana na ukurasa uliotangulia, chukua jambo moja ambalo unapambana nalo na uorodheshe hatua utakazochukua ili uweze kutii. Kutii katika jambo hili kutakuwezesha kuwa na uhusiano wa karibu na Yesu.

- Ukishalikomesha jambo hili, uliza Mungu ni hatua gani za kutii anazotaka uchukue kwa jambo lingine. Fanya hivyo mpaka uchukue hatua za kutii kwa kila jambo.

- Katika sehemu ya "Maswali Yanayo Ulizwa kwa Wingi" soma maswali na majibu juu ya "Kuwa na Uhusiano Wenye Kina na Kristo". Utagundua jinsi ya kutoa na kupokea msamaha, jinsi ya kubadili tabia mbaya, jinsi ya kukabiliana na shida tofauti katika maisha na jinsi ya kumjua Yesu zaidi.

- Endelea kuwa na wakati wa kimya kila siku na Mungu. Ukijipa muda, mazoea hayo yatasababisha uhusiano wa karibu na Yesu.

> Amri kuu ya kuelewa mambo ya kiroho si uwezo wa kufikiria bali kutii. Tendo la utiifu huja kwa ufahamu kumhusu Mungu Mwenye nguvu zote. ***Oswald Chambers***

# VIFAA VYA KUWA NA UHUSIANO WENYE KINA NA YESU

## Yesu Asiye na wa Kulinganishwa Naye





Barry St.Clair anakuelekeza kukutana na Yesu Kristo ili upate kumfahamu.

**Katika** *Yesu Asiye na Wakulinganishwa Naye,* utajipata katika barabara itakayokuongoza kumfanya Yesu kuwa rafiki mwema zaidi.

Katika kitabu hiki cha, *Yesu Asiye na Wakulinganishwa Naye,* Safari hii inakupeleka mwendo wa siku arobaini za kuzuru maisha,kifo, kufufuka, kupaa na kuja kwa pili. Mtazamo wako kumhusu Yesu utapigwa chenga na wewe utabadilika!


## Kuwa na Wakati wa Pekee na Mungu




Utaboresha vipi uhusiano wako na Kristo? Mda! Kama katika uhusiano mwingine wowote,, utapata kumfahamu Yesu vema kama utapata wakati wa kuwa Naye. Yesu ataka kusogelea karibu nawe unaposogelea karibu Naye. Kitabu hiki kitakusaidia kuwa na wakati na Mungu kila siku!

- Jifunze Biblia
- Tafakari Maandiko
- Furahia maombi
- Msifu kila wakati
- Mpe shukrani
- Kiri dhambi zako
- Jiombee
- Waombee watu wengine

**Agiza kutoka kwa tuvuti www.reach-out.org.**




# Kiini cha Habari

Tamanio la maisha la Dave Busby kumfuata Mungu laonekana wazi katika kitabu hiki. Baada ya kukiandika miaka minne kabla ya kufa kwake, kimeuzwa nakala 50,000. Sasa kimoboreshwa na mkewe Lawanna, ambapo kila sura imetangulizwa na matukio kutoka kwa kazi zake Dave ambazo zilikuwa bado zingali kuchapishwa. Maswali na mawazo ya ziada yanafuata kila sura na hivyo basi kukifanya kitabu hiki kuwa kizuri sana cha kujifunzia Biblia kwa vizazi vyote.

Dave Busby alikuwa wa ajabu. Katika udhaifu uliotokana na magonjwa mbalimbali kwenye mwili wake, alipata kupokea nguvu mpya inayodhihirisha 2 Wakorintho 12:10: “Kwa maana niwapo dhaifu ndipo ninazo nguvu.” Kusema kuwa Yesu ndiye aliyekuwa tumaini lake Dave si mzaha bali ndio ukweli wake uliokuwa wa kila siku. Usishangae kukumbana na uwezo wake Mungu unapouzuru ukweli wa mambo

**Agiza kwenye tuvuti www.reach-out.org.**

## Vitabu vingine vizuri

- *Abba’s Child* na Brennan Manning
- *Truefaced* na Bill Thrall, Bruce McNicol, pamoja na John Lynch
- *Emotionally Healthy Spirituality* na Peter Scazzero
- *The Sacred Romance* na Brent Curtis pamoja na John Eldredge

# MPANGO WA UTENDAJI

**Kwa sasa**, ...wafanya nini ili kuwa na uhusiano wenye kina na Kristo?

**Kupiga hatua,** ... Chukua yale umegundua na uunde mpango wa utendaji ili kuyashika na kuyafwata maono ya Huduma ya Vijana Inayomlenga Yesu.

**Kwa nini** ni muhimu wewe kuwa na uhusiano wenye kina na Kristo?

**Ni nini** utakachokifanya wewe ili kuwa na uhusiano wenye kina na Kristo?

**Ni nani** utakayewajibika kwake ili uwe na uhusiano wenye kina na Kristo?

**Ni wapi** utakapokutania na Kristo ili uwe na uhusiano wenye kina naye?

**Ni lini** na wakati upi utakaoutenga ili uwe na wakati mwema wa kuhusiana kwa kina na Kristo?

# Kuomba kwa Shauku

## Lengo

Kubuni Mazingira ya

Kuomba kwa Shauku

Sehemu ya Tatu

## KUMTAZAMA YESU

Kijana wangu ana shati ambalo limeandikwa, “Nikiwa ndani ya Yesu, mimi ni jinamizi wa kibinafsi wa shetani.” Kuomba kwa shauku kuna maana ya kuja karibu na Yesu na kumtazama akiusukuma nyuma ufalme wa giza wa shetani na kurudisha mahali pake ufalme wa Yesu wa nuru. Tusipoomba kwa shauku, shetani ni jinamizi wetu wa kibinafsi. Ufalme wa giza umeshika vijana kwa nguvu. Na kuomba kwa shauku ndio silaha ya kipekee ya kuachilia nguvu za Mungu kuwaokoa vijana kutoka kwa shimo na kuiweka miguu yao juu ya mwamba, kuwaondoa kutoka ufalme wa giza na kuwaleta katika ufalme wa nuru na hapo basi wanakuwa jinamizi binafsi la shetani.

Mwandishi wa Waebrania aliibuni picha ambayo inatuonyesha ni kwa nini kuomba kwa shauku lazima kuwe katika mstari wa kwanza katika maisha yetu kwa kuwakinga vijana wetu na maelfu ya vijana walio karibu nasi ambao wanamhitaji Yesu.

> *Hivyo, yeye anaweza daima kuwaokoa kabisa wote wanaomwendea Mungu kwa njia yake, maana yeye anaishi milele kuwaombea kwa Mungu (Waebrania 7:25).*

**Yesu aweza!** Kutoelewa kwetu ni ishara ya kukosa kuomba kwa shauku. Mwandishi wa Waebrania anaelewa hayo. Katika Waebrania 1:3, tunagundua kwamba Yesu anaweza kwa sababu:

- Ni “mrithi wa vyote.” Kutoka kwa Baba yake alirithi vitu vingi kumliko tajiri mkubwa Bill Gates na vingine vikabakia.
- Ni muumba – ambaye “kupitia kwake, Mungu aliumba ulimwengu.” Inachukua miaka 100,000 kusafiri kutoka pande moja ya nyota inayoitwa “Milky Way” mpaka upande wake mwingine. kwa mwaka mmoja inasafiri maili trilioni 5.88 na Milky Way ni galaksi (tufe) moja tu kati ya nyingi zingine, Yesu ni muumba ambaye anaweza yote.
- Ni kiangazia cha utukufu wa Mungu. Kumtazama Yesu ni sawa na kuitazama taswira/picha yake Mungu. Vyote alivyo Mungu, ndivyo alivyo Yesu.

- Yeye "amevishika vitu vyote kwa nguvu za Neno lake." Kwa neno lake, mamilioni ya viumbe kuanzia virusi hadi ndovu na trilioni za vifaa kuanzia galaksi/matufe hadi mfumo wa kiikolojia huidhinishwa naye.
- "Alitutakasa kutoka kwa dhambi." Kupitia kwa kumwaga damu yake alitufungulia njia ya utakaso – kuwa na uhusiano naye na kusamehewa dhambi zetu.
- Yeye anatawala kama "ameketi katika mkono wa kulia wa Mwenyezi Mungu." Baada ya msalaba na ufufuo, Yesu sasa ameketi katika mkono wa kulia akitawala ulimwengu mzima.

Uwezo wa Yesu ni wa kushangaza. Hapana shaka: Aweza "kuokoa kabisa"! Yesu hutumia uwezo wake kwa niaba ya wale "wote wanaomwendea Mungu kwa njia yake" (Waebrania 7:25).

Maombi ndicho chombo cha mawasiliano ambacho Mungu ametupa ili tuweze kusogelea karibu naye

**Twaweza kusogelea karibu**. Kwa sababu "tunaye Kuhani Mkuu aliyeingia mpaka mbinguni; Yesu, Mwana wa Mungu . . . Yeye mwenyewe alijaribiwa kama sisi kwa kila namna lakini hakutenda dhambi" Basi, tunaweza kumwendea Mungu kwa matumaini na kwa upendo. (Waebrania 4:1-17)

Tunapomwendea Mungu, tukiomba kwa shauku, tunajua kwamba, "yeye anaishi milele kutuombea kwa Mungu" (Waebrania 7:25). Tunaponena na Yesu, yeye hunena nasi kutoka mahali pake, mkono wa kulia wa Baba. Mtume Yohana alieleza taswira ya hali ya sala zetu mbele za Mungu.

*Moshi wa ubani ukapanda juu, pamoja na sala za watu wa Mungu kutoka mikononi mwake huyo malaika aliyekuwa mbele ya Mungu. Kisha, malaika akakichukua hicho chetezo, akakijaza moto wa madhabahuni, akakitupa duniani. Kukawa na ngurumo, sauti, umeme na tetemeko la ardhi*

***Ufunuo 8:4-5***

Badala ya kuomba baraka za Mungu kabla ya chakula tu, tumuombe Mungu abariki mikutano yetu baada ya kumpa mipango yetu au kuwa na maombi ya kufungua na kufunga mikutano ya vijana, Mungu anatuita "tumwendee". Tunapomwendea, tutagundua kwamba katika kiti chake cha enzi mna neema, mwelekeo, utambuzi, mtazamo, nguvu, motisha na matumaini au cho chote tukitakacho. Yote huja kwa kuomba kwa shauku!

## MASWALI MAGUMU

Tafakari maswali haya. Jiweke katika kiwango cha 1-10. Angalia jinsi umejibu maswali hayo. Andika aya fupi ukieleza kwa ukweli, uamuzi ambao unahitaji kuchukua kuhusu kuomba kwa shauku.

1. Je, unapenda kuomba kiasi gani?

   1 2 3 4 5 6 7 8 9 10

2. Kwa kiwango kipi waweza kuwa na nidhamu ya kuwa na wakati wako pekee na Mungu kila siku?

   1 2 3 4 5 6 7 8 9 10

3. Je, huwa mnakutana mara kwa mara na viongozi wengine kuwaombea wanafunzi wenu?

   1 2 3 4 5 6 7 8 9 10

4. Je, huwa mnakutana mara kwa mara na viongozi wengine kuomba katika chuo kilicho karibu?

   1 2 3 4 5 6 7 8 9 10

5. Ni asilimia ngapi ya wanafunzi wako ambao huwa na wakati wa kimya kila siku na Mungu?

   1 2 3 4 5 6 7 8 9 10

6. Ni asilimia ngapi ya wanafunzi ambao hujiunga na kundi ndogo la maombi kila juma?

   1 2 3 4 5 6 7 8 9 10

# KANUNI ZA HUDUMA YA VIJANA

**Je, tunawezaje kuongeza upendo wa kuomba kwa shauku na kubuni mazingira yatakayowafanya wengine kuomba kwa shauku?**

## Je, Wapenda Kuomba?

Je, unapenda kuomba? Au ni shughuli tu, wajibu au njia ya kupata kile unachotaka kutoka kwa Mungu?

> *"Penda kuomba. Kuwa na hamu ya kuomba mara nyingi kwa siku, na uchukue jukumu la kuomba. Maombi huongeza roho kiasi cha kuwa na uwepo wa kuchukua kipawa cha Mungu mwenyewe. Omba na utafute, na roho yako itaongezeka kiasi cha kumpokea na kumuweka yeye kuwa wako."*
>
> **( Mama Teresa)**

**Yesu Alipenda Kuomba!**

Tukitazama maisha ya Yesu kama mchezo wa kuigiza, Yeye ni mhusika mkuu (maarufu), wengine wote ni wahusika wasaidizi na maombi ni pazia ya nyuma ya jukwaa.

**Alianza kwa maombi**. (Luka 3:21-22)

**Aliendelea kwa maombi.** (Yohana 5:19)

**Aliomba kila siku**. (Marko 1:35)

**Aliomba kabla ya kufanya uamuzi mkuu au tukio**.

| | | | |
|---|---|---|---|
| Luka 6:12-13 | Kuwaita wanafunzi wake, | Luka 9:16 | Kuwalisha watu 5000 |
| Mathayo 15:36 | Kuwalisha watu 4000, | Mathayo 14:22-23 | Kutembea juu ya maji |
| Yohana 11:41-42 | Kumfufua Lazaro, | Mathayo 26:26-29 | Karamu ya Bwana |

**Aliendeleza maisha yake yote na huduma kwa maombi**. (Luka 5:16).

**Alimalizia kwa maombi**. (Luka 22:39-44, Luka 23:46)

**Anaendelea kuomba**. (Waebrania 7:25)

*"Bwana Yesu bado anaomba. Miaka 30 ya kuishi, miaka 30 ya huduma, tukio moja la kufa. Miaka 2000 ya maombi. Je, huo ni mkazo wa maombi wa aina gani."*

**S.D. Gordon.**

Yesu alikuwa na shauku ya kuwasiliana na Baba yake. Anataka tuwe na upendo huo huo wa kuwasiliana na Baba Yetu aliye mbinguni.

## Je, Wewe huhisi Uwepo wa Nguvu za Mungu?

**Bidii Zetu Zote Hazina Nguvu Yoyote**

"Maombi si tu faida kubwa kwetu na furaha isiyokuwa na kifani . . bali ni silaha iliyo na matokeo ya kupokea. Mengine yote hutuacha tukitatanika katika machafuko na vurugu za bidii za kibinafsi, ambazo hazijawahi kuwa na matokeo yoyote ila kichochorochunge au hutuacha katika maisha ya udhaifu bila mwelekeo, bila dira, bila rubani. Tunapojenga bila mwongozo kutoka kwa aliye juu, ambaye huongoza kulingana na mpango wa milele, kazi yetu, hata iwe nzuri namna gani, itakuwa ya bure. (F.J. Huegel, "Maombi: Faida Yetu Kuu," Decision, June, 1996.)

### Uwezo Mwingi katika Bidii Ndogo ya Mungu

Si vigumu kuelewa uzito wa 'nguvu/uweza' . Mungu asema kupitia kwa Yeremiah

*"Niite, nami nitakujibu na kukuambia mambo Makubwa yaliyofichika ambayo hujapata kuyajua"*
Yeremia 33:3

Tunapoomba ("Niite") Mungu hutupa ahadi ("Nami nitakujibu") kwamba atadhihirisha nguvu zake kwetu ("na kukuambia mambo makubwa yaliyofichika ambayo hujapata kuyajua").

Charles Spurgeon alipenda kuzunguka kanisa lake kabla ya ibada. Alipenda kupeleka washiriki wake katika chumba cha chini kabisa cha kanisa. "Hapa nataka muone nguvu za msingi wa kanisa," alisema. Wakati Spurgeon aliufungua mlango na kuuweka wazi, kwa ghafla, hapo ndani waliwaona wanaume na wanawake waliojaa chumbani wakiwa kwenye magoti wakiomba.

*Tazama huduma yako ya vijana kama chumba hicho kilichojaa watu.*

## Wawezaje Kuendelea Kuomba kwa Shauku?

1. **Kwa kuwa na wakati wa kimya kila siku peke yako na Mungu.**

Kuwa na wakati wa kimya peke yetu kila siku, huzidisha upendo wetu, hisia zetu, na uhusiano wetu na Mungu. Kutoka Ibrahimu hadi Musa, Mtume Paulo . . . hadi kwetu sisi, kuwa na wakati wa kimya na Mungu ni nidhamu ya kipekee katika maisha ya mkristo. Mungu anataka tuanze sasa!

*Kama hakuna Biblia,*
*Hakuna kifungua kinywa.*

2. **Kwa kuomba na wengine.**

Uwezo wote wa Mungu ulio mbinguni anatoa kwetu sisi bure. Maombi yetu ndiyo huamua kama tutapata au la. Hiyo ni nguvu!

*"Nawaambieni kweli, mtakachokifunga duniani kitafungwa mbinguni, na mtakachokifungua duniani kitafunguliwa mbinguni. Tena nawaambieni, wawili miongoni mwenu wakikubaliana hapa duniani kuhusu jambo lolote na kuomba, Baba yangu wa mbinguni atawafanyia jambo hilo. Kwa maana popote pale wanapokusanyika wawili au watatu kwa jina langu, mimi nipo hapo kati yao"*

***Mathayo 18:18-20***

Nguvu zake huachiliwa tunapoomba tukiwa “wawili au watatu”.
Tutawezaje kuomba wawili au watatu ambavyo Yesu anatuhimiza tufanye?
Jaribu kuitafakari sentensi ifuatayo na uweza wa maneno yake Kristo. ‘kwani walipo wawili au watatu katika Jina langu, papo hapo nitakuwa nao’

Kutana { na Wakristo wa
Mara **3** kwa juma kuomba kwa ajili ya
Watu wa wasio Wakristo

Tunaweza kukubaliana wawili au watatu – anavyo tuhimiza Yesu. Katika hatua za utendaji, utaandaa mkakati wako wa maombi ya watatu.

**MAOMBI HUACHILIA NGUVU ZAKE YESU KUPITIA KWAKO ILI KUWABADILISHA WATU!**

# HATUA ZA UTENDAJI

Kuwa na upendo wa kuomba kwa shauku hutuongoza kwa hatua za utendaji.

- Kariri Yohana 5:19

- Panga kutumia dakika 20 kila siku peke yako na Mungu mpaka yawe mazoea. Tumia kijitabu cha *Wakati wa Kimya na Mungu* kama mwongozo, kutoka kwa mfululizo wa vitabu vya *Kuelekea Katika Kukua* (series of Moving Towards Maturity).


- Karibisha viongozi wengine wa vijana, ikiwezekana kutoka makanisa mengine au dini zingine, ili muweze kuomba mkiwa kundi la maombi la watatu ndani ya chuo/shule/kanisani mwenu.

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **OMBI LA WATATU** | **KUTANA** | Na Wakristo | 3 | 1.________________ 2.________________ 3.______________ |
| | | Mara | | **Kwa juma**<br>Jumatatu*Jumanne*Jumatano*Alhamisi*Ijumaa*Jumamosi *Jumapili |
| | | Kuombea watu | | **Wasio wakristo**<br>1.________________ 2.________________ 3.______________ |

- Hamasisha wanafunzi wako kuomba kwa shauku kwa kuwafundisha jinsi ya kuwa na wakati wa kimya na Mungu. Tumia kijitabu cha *Wakati wa Kimya na Mungu* kama mwongozo kutoka kwa mfululizo wa vitabu vya *Kuelekea katika Kukua* (series of Moving Towards Maturity.)

Hamasisha wanafunzi wako kuomba kwa shauku kwa kuwaandaa kwa maombi katika vikundi vya watu watatu watatu. Tumia jinsi ya kuomba katika kundi la watatu kama ilivyoandikwa katika kijitabu cha '*Njia ya ajabu ya Kuomba'*

# VIFAA VYA KUOMBA KWA SHAUKU




## Wakati wa Pekee na Mungu

Wewe hufanya nini unapokuwa na wakati wako pekee na Mungu? Unaongea na kusikiza! Unanena na Mungu na kumruhusu kunena nawe. Kama unapata shida kuamuka, mchovu na asiyejua la kutenda, basi hiki ni kitabu chako. Kita:

- kuchochea asubuhi kuamka na kuwa na wakati na Mungu.
- kuandaa kwa wakati huo na Mungu.
- sababisha Biblia kuwa hai katika mtazamo wako.
- kukutanisha na Mungu kupitia mpango mwepesi.

## Njia ya Ajabu ya Kuomba




Wanafunzi watafurahia kuishi maisha, kuwapenda rafiki zao, na kuelezea habari zao kupitia maombi. Kusisitiza kwa majuma haya manane kutabadilisha maisha yao, vyuo vyao, na huduma yao ya vijana kupitia kwa maombi.

Kijitabu chenye kurasa 80 cha wanafunzi kinatolewa bure na chaweza kupatikana kwenye tuvuti.

*Mwongozo wa Viongozi* kinakupa sehemu nane za masomo ya makundi pamoja na vijitabu, mawazo na matendo mbalimbali.

**Agiza kwenye tuvuti www.reach-out.org.**

## MPANGO WA UTENDAJI

MPANGO WA UTENDAJI WA KUOMBA KWA SHAUKU

**Kwa sasa**, ...wafanya nini ili kuomba kwa shauku

**Kupiga hatua,** ... Chukua yale umegundua na uunde mpango wa utendaji ili kuyashika na kuyafuata maono ya *Huduma ya Vijana Inayomlenga Yesu.*

**Kwa nini** ni muhimu wewe na wenzako katika huduma yako kuomba kwa shauku?

**Ni nini** mtakachokifanya wewe na wenzako katika huduma yako ili muombe kwa shauku?

**Ni nani** atakayejiunga nanyi katika kikundi chenyu cha watatu, na ni nani katika huduma yako atakayeanzisha vikundi vingine vya watatu watatu?

**Ni wapi** kikundi chenyu cha watatu kitakapokuwa kikikutania kwa kuomba?

**Ni lini** kikundi chenyu cha watatu kitakuwa kikikutana kwa maombi?

# Kuwaandaa Viongozi

## Lengo

Kuwaandaa Viongozi Wenye sifa

Bora  Kwa ajili ya Huduma Yenye

Kina na ya Muda Mrefu

Sehemu ya nne

# Kuwaandaa Viongozi

4

## KUMTAZAMA YESU

Katika uongozi, kwa watu wengi, njia rahisi huwa ni kutumia yule ambaye utampata kibahati. Ukimchukua yeyote anayeonekana kama kwamba ana sifa za uongozi na umpatie cheo, uongozi unakuwa kama mazoezi katika mpangilio. Hii ni tofauti kabisa na utaratibu wa uongozi wake Yesu!

Tunapochunguza watu ambao Yesu alichagua kuwa wanafunzi wake kumi na wawili, ni kundi lisilo la kawaida na bila matumaini ya kufaulu. Yesu alijua jambo juu yao ambalo mtu wa kawaida hangeweza kuliona. Ni nani angemchagua mtoza ushuru ambaye alifanya kazi Roma (Mathayo), na shabiki (Simioni) ambaye lengo la maisha yake lilikuwa kuharibu Roma. Tafakari kongamano la watu hao wawili! Na je, Thomasi – ambaye hakuamini jambo lolote? Au Petro ambaye alikuwa mchochezi? Kulikuwa pia na Yuda, msaliti. Rekodi za kihistoria zaonyesha kwamba wengi wao walikuwa vijana wadogo. Ni kanisa gani laweza kuruhusu vijana kuwaongoza? Yesu alikuwa na mawazo gani?

Hatuwezi kujua kwa kweli. Lakini, jambo moja li wazi. Wakati alikamilisha miaka mitatu ya mafundisho ya viongozi na kundi hili la watu wa kiwango cha chini, "walibadilisha ulimwengu." Ni jambo gani tunaloweza kujifunza kutoka kwa Yesu, ambalo litatupa changamoto ya kuandaa viongozi ambao watabadilisha ulimwengu?

***Vipande vilivyopondekapondeka***. Yesu alipotazama ndani ya roho za watu kumi na wawili ambao alitaka kuwaita, aliona kiburi, ujeuri na watu walio na nguvu za kimwili. Lakini baada ya miaka mitatu walikuwa watu waliovunjika, waliotazama ndoto zao zilizoharibika kabisa na kushangaa, "Sasa, kwa sababu haya yamekwisha, tufanye nini?" Walijificha katika chumba cha juu wakihofia maisha yao, kwani walijua hawawezi kufanya jambo lolote kubadilisha hali yao. Yesu aliwapeleka mpaka mwisho wa maisha yao ili waweze kutambua kwamba uongozi si, ". . . kwa nguvu au kwa uwezo wako mwenyewe, bali ni kwa msaada wa roho wangu.' Mimi Mwenyezi Mungu wa majeshi nimesema" (Zekaria 4:6).

Baadaye ndipo Yesu alisema, "mtapokea nguvu . . ." (Matendo 1:8). Uongozi utakua ndani yetu tukikubali msalaba, tukiruhusu Yesu atupondeponde na kutupa umbo jipya na kuwa watu ambao wanaonyesha sifa zake. Viongozi wetu watakua wakikumbatia msalaba, wakiwa katika hali ya kuvunjika na wakiruhusu Mungu awape umbo jipya. Katika kundi la viongozi, ruhusa imetolewa ya kuvunjwa huko na kupewa umbo jipya.

***Kukesha Usiku Kucha.*** Yesu hakuchukua uamuzi wa kuchagua wanafunzi kumi na wawili kwa urahisi. Luka anatwambia, ". . . Yesu alikwenda mlimani kusali, akakesha huko usiku kucha akisali" (Luka 6:12). Hiyo ilikuwa kabla ya kwenda kuwachagua wale kumi na wawili siku iliyofuata. Mtu mmoja alisema, "Wakati mwema wa kumuachisha mtu kazi ni kabla ya kumpa kazi." Hii ina maana kuwa, "Njia bora ya kuzuia kuwa na viongozi wabaya ni kutowachagua." Lakini njia ya pekee ya kujua kama ni viongozi wema ni kuuleta uamuzi mbele za Mungu, na kwa maombi mengi, mwache achague. Kundi la viongozi litafaulu kama ulimwomba Mungu akupe viongozi wema na umeendelea kumwomba akuonyeshe yale utakayotenda kuwahusu.

***Kutoa Maono***. Yesu alichagua wale kumi na wawili. Lakini kwa kweli walimchagua. Aliwaambia, "Nifuateni, nami nitawafanya nyinyi kuwa wavuvi wa watu" (Mathayo 4:19). Tia maanani kwamba alimuita kila mtu kibinafsi au akiwa katika kundi la watu wawili, lakini hakuita kundi lote mara moja. Aliwapa changamoto ana kwa ana. Wakati huo, kila mmoja ilimbidi afanye uamuzi wake kumhusu. Changamoto kwao ilihusu maono yake kwao. Kwanza, jambo la muhimu zaidi, alitaka wanafunzi wake "wamfuate." Huu ni muhtasari wa uongozi wa mambo ya kiroho. Si mambo ya kupata watu wa kujaza nafasi ili tuwatumie kuwa viongozi wa vijana. Lakini ni juu ya kujenga, kulea na kutia watu moyo katika uhusiano wao na Kristo. Hiyo itawapa yale wanayohitaji ili waweze kuongoza wanafunzi vyema. Jambo la pili, Yesu aliagiza wanafunzi wake kuwa watakuwa "wavuvi wa watu." Hakuwaita kuwa "waweka tangisamaki". Changamoto ya Yesu ya ana kwa ana kwa wanafunzi wake haikuwa ya kujenga shirika au kuongeza nambari, bali kubadilisha ulimwengu! Maono yake yalikuwa rahisi na wazi. Twaweza kuwapa viongozi wetu changamoto ili wawe na maono sawa na yale ya Yesu.

***Sheria ya Uhusiano***. Yesu alijua umuhimu wa uhusiano. Katika maisha yake yote alikuwa amekaa katika uhusiano mwema na Baba na Roho Mtakatifu. (Hilo ni kundi ndogo halisi). Kwa hivyo aliwaita hawa kumi na wawili waweze kuwa na uhusiano naye kama vile alivyokuwa na uhusiano mwema na Baba na Roho Mtakatifu. Kwa miaka mitatu iliyofuata, mwelekeo wake ulikuwa kwa watu hawa. Alikuwa na uhusiano mwingine wo wote? Ndiyo. Alinena na makundi makubwa? Twajua alinena nao. Lakini mwisho wa kila siku, baada ya uhusiano wake na Baba, alihusika sana na hawa kumi na wawili. Viongozi wa vijana, wanapenda watoto. Na uwezo wetu wa kuhusika nao ndio sababu tunafanya kazi nao. Lakini, tunaweza kuwa na uhusiano bora na kikundi cha watu wangapi? Kwa kweli si zaidi ya kumi na mbili. Tukitazama huduma ya Yesu na tutake kuunda zetu kama yake, na kama tunaamini kwamba vijana hubadilishwa kupitia kwa uhusiano, basi ni lazima tuandae kundi la viongozi kama vile Yesu alivyofanya. Na hapo tutazalisha na

kuongezea huduma zetu kupitia kwa viongozi wakomavu tunaowaandaa na kuwawezesha.

***Kusawazisha Matendo***. Yesu aliwachagua watu wale, si kwa sababu walikuwa sawa lakini kwa sababu walikuwa tofauti. Walikuwa tofauti sana katika nafsi zao. Lakini Yesu alipendezwa na hayo. Aliwachagua pia kwa sababu ya tofauti zao za vipawa vya kiroho. Yesu aliruhusu nafsi zao na vipawa vyao kuleta wasiwasi katika kundi. Lakini, alijua kuwa watu hawa walikuwa na mchanganyiko mwema wa vipawa vya kiroho ili waweze kutoa usawa kwa kanisa jipya na changamoto ambayo itaenea baada ya kupaa kwake. Kwa mfano Petro alikuwa Mtume . . . "juu ya mwamba huu nitalijenga kanisa langu", na Filipo alikuwa mwinjilisti. Hakuna kiongozi hata mmoja wa vijana ambaye ana vipawa vyote. Viongozi wengi wanahitajika ili walete usawa katika huduma ya vijana. Baada ya vipawa hivyo kujitokeza ndipo uongozi wetu utapata usawa. Usawa huo utakuja pamoja na nguvu za Roho Mtakatifu za kufanya huduma ya Yesu Kristo.

***Kuekeza katika Wakati***. Baada ya Yesu kuwachagua wanafunzi wake, alianza kuwa na wakati mwingi nao. Tukilinganisha miaka mitatu ya wakati ambao Yesu alitumia pamoja na wanafunzi wake dhidi ya wakati ule alioutumia na kundi kubwa la watu, utagundua kwamba aliutumia muda mwingi na tena bora kabisa na wanafunzi wake. Alianza kwa kutumia wakati wake mwingi na kundi kubwa la watu, lakini wakati ulipoendelea, alianza kutumia wakati mwingi na wanafunzi wake. Alipokuwa karibu kufikia mwisho wa huduma yake hapa duniani, alitumia wakati wake wote na wanafunzi wake. Leo hii, sherehe na matendo ndiyo huendeleza huduma nyingi za vijana. Ili kuandaa viongozi kama wale Yesu aliowaandaa, ni lazima hayo yabadilike. Ni lazima tutumie wakati wetu mwingi kuwaandaa viongozi ambao watawaandaa vijana. Hiyo ndiyo njia ya pekee ambayo itasababisha huduma kuenea kwa kina na kukua.

***Kuzidisha Kukua***. Yesu alipokuwa akitoa wakati wake kwa wanafunzi, alikuwa na Amri Kuu katika mawazo yake. Injili zote nne zimeandika hayo, pamoja na kitabu cha Matendo.

> *"Nimepewa mamlaka yote mbinguni na duniani. Nendeni basi, mkawafanye watu wa mataifa yote wawe wanafunzi wangu, mkiwabatiza kwa jina la Baba, na la Mwana na la Roho Mtakatifu. Wafundisheni kushika maagizo yote niliyowapeni. Nami nipo pamoja nanyi siku zote; naam, mpaka mwisho wa nyakati".*
>
> *Mathayo 28: 18-20*

Hayo ni kulingana na Injili ya Mathayo (Mathayo 28:18-20). Injili zingine ambazo zimeandika ni; Marko 16:15-16, Luka 24:4-49, Yohana 20:21-22 na Matendo 1:8. Chini ya mamlaka ya Yesu, mahali popote walipoenda wanafunzi wa Yesu walitakiwa kuwafanya wanafunzi. Wanafunzi hao wangewafanya wengine kuwa wanafunzi na waendelee mpaka kanisa lifanye "watu wa mataifa wote kuwa wanafunzi." Kwa pesa, vifaa, maandishi, na wahubiri wa televisheni tulio nao, tunatakiwa tuwe tumemaliza kazi wakati kama huu. Lakini hatujamaliza. Kwa nini? ***Kwa sababu tumepoteza mwelekeo wa amri ya Yesu ya kuwaandaa viongozi kwa kuwafanya wanafunzi***. Badala ya kuzidisha wanafunzi tumekuwa tukizidisha washiriki wa kanisa bila kuwafanya wanafunzi.

Tukifanya hesabu, itafanana hivi na vilevile kama tukifuata maono ya Yesu ya kuwaandaa viongozi kwa kuwafanya wanafunzi basi kuongeza kutabadilika na kuwa kuzidisha kama ilivyo katika jedwali hili:

| **MWAKA** | **WASHIRIKA ( +)** WATAKAVYOONGEZEKA | **WANAFUNZI** (X) WATAKAVYOZIDI |
|---|---|---|
| Mwaka wa **Kwanza** | **1** | **1** |
| Mwaka wa **Pili** | **2** | **2** |
| Mwaka wa **Tatu** | **4** | **6** |
| Mwaka wa **Nne** | **8** | **18** |
| Mwaka wa **Tano** | **16** | **54** |
| Mwaka wa **Sita** | **32** | **162** |
| Mwaka wa **Saba** | **64** | **1,458** |
| Mwaka wa **Ishirini na moja** | **1,048,576.** | **7,016,615,523.** |

Katika sehemu ya washirika, tambua kwamba mtu mmoja akiongeza mtu mmoja kwa mwaka, basi kutakuwa na watu 1,048,576. Ilhali sehemu ya uanafunzi inaonyesha mambo yatakavyokuwa kama mtu mmoja akimfuasa mtu mmoja mwingine kwa mwaka kisha wawili wawafuase wawili zaidi mwaka utakaofuata; sita hao wawafuase sita wengine kila mmoja, na waendelee jinsi hiyo kila mwaka. Kwa kuzidisha, idadi ya wanafunzi itafikia watu bilioni 7 katika miaka 21 ambayo ni idadi zaidi ya watu bilioni 6.8 waliomo duniani kwa sasa. Wote hao wakiwa wamepatikana kwa shinikizo la mtu mmoja.

Kama mtu mmoja anaweza kumfanya kiongozi mmoja kwa uanafunzi kila mwaka, basi kwa njia ya kuzidisha watu zaidi ya bilioni tano watakuwa wanafunzi wa Yesu kwa miaka 32. Hao ni watu wote wa dunia wakabakia milioni moja tu! – wote kupitia kwa mtu mmoja. Je, kutakuwaje, ukizidisha watu 12 kwa njia hiyo kupitia kwa kundi lako la viongozi?

Yesu alijua njia inayofaa kabisa ya kutimiza Amri Kuu ("Mpende Mungu wako") na Wito Mkuu ("kufanya watu wa mataifa"). Jambo la ajabu ni kwamba ametuita tufanye hivyo!

## MASWALI MAGUMU

Tafakari maswali haya. Jiweke katika kiwango cha 1-10. Angalia jinsi umejibu maswali hayo. Andika aya fupi ukieleza mahitaji yako ya kibinafsi ya uongozi na ya uongozi wa huduma yako.

1. Je, una uwezo kiasi gani wa kuathiri - watu waliojitolea, wazazi wako na wanafunzi?

   1 2 3 4 5 6 7 8 9 10

2. Je, watu waliojitolea wana hamu ya kufundishwa mpaka kiwango gani?

   1 2 3 4 5 6 7 8 9 10

3. Je, una hamu ya kufundisha watu waliojitolea mpaka kiwango gani?

   1 2 3 4 5 6 7 8 9 10

4. Kwa jumla, watu wazima waliojitolea wamekubali wajibu wao kwa Kristo kwa kiwango gani?

   1 2 3 4 5 6 7 8 9 10

5. Je, ni kwa kiwango kipi watu wazima waliojitolea wana wajibika katika uhusiano wao?

   1 2 3 4 5 6 7 8 9 10

6. Je, watu wazima waliojitolea wanawajibika kiasi kipi katika huduma yao kwa vijana?

   1 2 3 4 5 6 7 8 9 10

Mahitaji yangu ya uongozi kibinafsi na ya huduma.

# KANUNI ZA HUDUMA YA VIJANA

Wawezaje kuwaandaa viongozi wenye sifa bora kwa huduma yenye kina na ya muda mrefu?

## Kusudi La Kundi la Viongozi

Katika Yohana 17:20-26 Yesu aliwaombea wanafunzi wake kwa Baba yake juu ya mahitaji haya.

- Wajitolee kwake Kristo
- Wajitolee, mmoja kwa mwingine
- Wajitolee kuwahudumia wanafunzi

Kutokana na yale Yesu amesema hapo juu, utaweza kueleza vipi malengo ya kikundi chako cha uongozi?

***Uongozi ni kuwa na uwezo wa kuathiri !***

***Kiongozi:***

- ***Anajua anakoelekea***
- ***Ana watu wanaomfuata***

# Hatua endelezi za kikundi cha  Uongozi

Tukitazama muda wote wa miaka mitatu ya huduma yake Yesu,  tunapata kutambua kwamba Yesu aliwaandaa wanafunzi wake hatua kwa hatua hadi hatua nne,  mara kwa mara akizichanganya hatua hizo. Hata hivyo hatua zote nne zililenga jambo moja. Tafakari maandiko katika kila hatua na uone kama waweza kuligundua.

Hatua nne za Yesu za kuwaandaa viongozi

**Natenda**.  ( Luka 4: 31-37 na 38-44)

**Natenda na wako pamoja nami.**  (Luka 5: 1-11)

**Wanatenda na niko pamoja nao.**  (Luka 10: 1-17)

**Wanatenda na niko nyuma yao kuwapa motisha**.   (Luka 24: 44-49 na Matendo ya Mitume yote)

# Nguvu katika "tenda"

Tukitazama neno "tenda" katika ukurasa uliotangulia, maana yake ni nini?

**Masihi atakuja "Kutenda" (Isaya 61:1-3)**

*Bwana Mwenyezi-Mungu amenijaza roho yake,*
*maana Mwenyezi-Mungu ameniweka wakfu, akanituma niwaletee wanaokandamizwa habari njema,*
*niwatibu waliovunjika moyo,niwatangazie mateka kwamba watapata uhuru,*
*na wafungwa kwamba watafunguliwa.*
*Amenituma niutangaze mwaka wake wa neema,na siku ya Mungu wetu ya kulipiza kisasi;*
*niwafariji wote wanaoomboleza;*
*niwape wale wanaoomboleza katika Sayuni taji la maua badala ya majivu,*
*na mafuta ya furaha badala ya maombolezo,*
*vazi la sifa badala ya mopyo mzito.*
*Nao wataitwa mialoni mathubuti,*
*aliyopanda Mwenyezi-Mungu kuonyesha utukufu wake.*
***Isaya 61:1-3***

**Yesu Alikuja Kama Masihi na "Akatenda" Luka 4:18-19**

*Roho wa Bwana yu juu yangu,*
*kwani ameniweka wakfu*
*niwaletee maskini Habari Njema.*
*Amenituma niwatangazie mateka uhuru wao,*
*na vipofu watapata kuona tena;*
*amenituma niwakomboe wanaoonewa,*
*na kutangaza mwaka wa neema ya Bwana.*
***Luka 4:18-19***

**Wanafunzi "Walitenda" (Marko 6:12-13)**

*Basi wakaondoka, wakahubiri watu watubu. Waliwafukuza pepo wengi wabaya; wakawapaka mafuta wagonjwa wengi wakawaponya.*

**Sasa "Tunatenda" (Yohana 14:12)**

*Kweli nawaambieni, anayeniamini atafanya mambo ninayoyafanya mimi; naam, atayafanya hata makuu zaidi, kwani ninakwenda kwa Baba.*

## "tenda" ina maana gani?

Yesu alisema kuwa sisi "Mtayatenda yale nimekuwa nikiyatenda." Yesu alikuwa akifanya nini?

Ni huduma yake Yesu itendayo

- Inahubiri habari nzuri
- Inawaponya wagonjwa na waliovunjika mioyo
- Inawafunguwa waliotekwa nyara na shetani

Baada ya kumjua Yesu, faida kubwa ambayo viongozi wa vijana wanayo ni kuileta huduma ya Yesu kwa wanafunzi au vijana walio na njaa, wanaoumia na wasio na tumaini.

# HATUA ZA UTENDAJI

Tafakari kuhusu kundi la viongozi ambalo lina uhusiano wa karibu na Yesu na linalotoa maisha yalo kwa vijana. Chukua hatua nyingine zaidi ya hapo. Fikiria juu ya kundi la viongozi ambalo limeandaliwa "kufanya hivyo." Wanaweza kuhubiri Habari Njema, kuponya waliovunjika moyo, kuwaweka huru waliotekwa. Ajabu! Maono hayo yaweza kuwa kweli tu kama ukichukua hatua zifuatazo.

1. **Omba**

   Kuwa na muda wa kuomba kwa dhati ili kufahamu ni nani ambaye Mungu anamuita kujiunga na kundi lako la viongozi.

2. **Ongoza**

   Unaweza kuwakilishwa katika kazi nyingi zingine, lakini kazi ya uongozi si moja wapo. Kiongozi wa vijana lazima aliongoze kundi la uongozi.

3. **Chagua.**

   Waweza kuchagua timu ya viongozi wako kutoka kwa watu tofauti: viongozi wa vijana walioko wakati huu, wazazi wa vijana wadogo, wanafunzi wa chuo na wengineo ambao wanapenda vijana na Mungu amewaita kufanya kazi nao. Mpe kila mmoja changamoto ya kuwa katika kikundi cha uongozi.

4. **Kabidhi**

   Unapotoa changamoto kwa mtu binafsi, mueleze maono yako ya huduma ya vijana na uyatie kwenye maandishi ili ayanakili. Fafanua na ueleze kujitoa kwako kwa uongozi wa kundi. Wanahitaji kujua yale watakayoyatarajia wanapoanza. (Tazama ukurasa wa nne wa ***Kutembea na Yesu Kibinafsi***. *(A Personal Walk with Jesus))*

5. **Jitayarishe**

   Pitia kila sehemu ya mafundisho kabla ya mkutano. Kwa maombi jitayarishe kwa mkutano kwa kusoma "Mwongozo wa Majadiliano" katika kila kitabu cha "Kuandaa Viongozi". Kujitayarisha kwako ni muhimu na kutaleta tofauti kubwa katika majadiliano!

6. **Kuwa na Mikutano**

Kuwa na wakati wa kukutana. Mikutano huwa inasaidia watu wengi. Ikiwezekana panga kukutana katika nyumba ya mtu mmoja. Kutana mfululizo kwa muda wa saa moja hadi moja u nusu. Tumia dakika 15 kwa maombi, dakika 45 kwa majadiliano na dakika 15 kuomba juu ya maudhui ya huduma ya vijana.

7. **Ekeza**


Kuekeza wakati na raslimali katika maisha ya watu hawa itawafanya wamjue Yesu, vipawa alivyowapa, na jinsi ya kuekeza vipawa hivyo katika maisha ya vijana.

8. **Tathmini**

Baada ya kila mkutano wa kundi tathmini yale mliyoyafanya na jinsi ya kuyafanya yawe mazuri zaidi. Tatua matatizo na ufanye marekebisho unapostahili.

# VIFAA VYA KUWAANDAA VIONGOZI – KWA WALIOJITOLEA

## Mfululizo wa vitabu vya *Kuwaandaa Viongozi*




Mfululizo wa vitabu vya Kuwaandaa Viongozi unakupa mapangilio wa utendaji wa kibiblia wa kuwaandaa viongozi waliojitolea. Watapokea motisha, maono na ujuzi wa kufanya uhusiano na kuwafuasa wanafunzi – na vilevile kumtangaza Kristo Kwa vijana wasioamini. Vitabu hivi vya mafungu matatu vinajumlisha sehemu 12 katika kila kitabu na kinaingiliana na ratiba ya kanisa lako kwa urahisi

**Kutembea kibinafsi pamoja naye Yesu Kristo** (kitabu cha kwanza) huwaelekeza viongozi kukuwa kwa kina naye Yesu Kristo

**Maono kwa maisha na huduma** (kitabu cha pili) hupanua maono ya kiongozi wako kwa ajili ya maisha na huduma yao.


**Vifaa muhimu kwa uongozi wa vijana** (kitabu cha tatu) kinawapa viongozi wako ujuzi wa kuwaathiri wanafunzi.

**Mfululizo wa vitabu vya Kuwaandaa Viongozi** (mafungu matatu) vina **Kutembea kibinafsi pamoja naye Yesu Kristo** (kitabu cha kwanza), **Maono kwa maisha na huduma** (kitabu cha pili) na **Vifaa muhimu kwa uongozi wa vijana** (kitabu cha tatu)

**Fungu la kusikiza** lina jumbe 6 ambazo zaweza kupatikana kwenye tuvuti. Vimefanywa nao Barry St. Clair, Dave Busby, pamoja na Louie Giglio.

**Agiza kutoka tuvuti www.reach-out.org.**

# VIFAA VYA KUWAANDAA VIONGOZI – KWA UZAZI



## Kichochezi cha Wazazi

Kitabu hiki kinawaandaa viongozi wa vijana wa kwanza – wazazi! Wazazi wanapata nafasi ya kufahamikiana na watoto wao. Wanapokipitia kitabu, wanagundua jinsi ya kumpenda Mungu kutoka katika mioyo yao na kuwaongoza watoto wao kufanya vivyo hivyo. Wazazi wanatambua jinsi ya kuekeza kiroho katika watoto wao kwa kuwafuasa na kuwafuasa marafiki za watoto wao.

## Kifaa cha Kuwachochea Wazazi

*Kifaa cha kuwachochea wazazi* kinapeana kwa makanisa mpango mwepesi wa kiutendaji wa kuwaandaa wazazi. Fungu hili lililo kami;lika huongoza makundi ya wazazi kupitia Kifaa cha Kuwachochea Wazazi. Masomo haya yanajumlisha:



- **kitabu** hiki kinawapa wazazi mbinu mpya ya kuwaelewa watoto wao
- **kijitabu** kinachowasaidia wazazi kutekeleza yale wanayoya gundua katika kifaa
- **CDs** za kusikiza zinazo wapa motisha
- **DVDs,** zikiwemo 6 za dakika 55 kila moja za mijadala na wazazi mbalimbali wakielezea changa moto zao na kufaulu kwao

**Mwongozo wa Viongozi** wa kuanzisha nam kuongoza kundi ndogo



## Fungu la Wazazi

*Kifaa cha kuwachochea wazazi* kinawapa raslimali 3 ambazo wazazi huhitaji ili kutumia vizuri zaidi katika jamii.

**Agiza kutoka kwa tuvuti www.reach-out.org.**

# MPANGO WA UTENDAJI

**Kupiga hatua**, ... *Chukua yale umegundua na uunde mpango wa utendaji ili kuyashika na kuyafwata maono ya Huduma ya Vijana Inayomlenga Yesu.*

**Kwa sasa**, ...wafanya nini ili kuwaandaa viongozi?

**Kwa nini** ni muhimu kuwaandaa viongozi?

**Ni nini** utakachokifanya ili kuwaandaa viongozi?

**Ni nani** hao viongozi utakaowaandaa?

**Ni wapi** utakapokutania na kikundi chako cha viongozi?

**Ni lini** utakapoanza na kuendelea kukutana na kikundi chako cha viongozi?

# Uanafunzi

## Lengo

Kufanya uanafunzi kwa wanafunzi/vijana hadi wahisi mabadiliko maishani mwao ili nao waweze kuwabadilisha wengine.

**Sehemu ya tano**

## KUMTAZAMA YESU

Katika historia yote, Mungu amefanya kazi muhimu kupitia kwa watu wachache zaidi kinyume na watu wengi. Yesu alipojikabidhi kwa kundi ndogo la wanafunzi kwa muda mfupi "walibadilisha ulimwengu juu chini" (Matendo 17:6). Tukitazama jinsi Yesu alivyojihusisha katika maisha ya wanafunzi wake inatupa mwelekeo halisi wa jinsi ya kutekeleza kazi muhimu ya uanafunzi.

**Chagua.** Uanafunzi ulianza kwa ***kuwachagua*** wanafunzi. Katika Luka 6:12-19, tunaona kwamba "Yesu alikesha usiku kucha akisali" (6:12). Kesho yake, "aliwaita wanafunzi wake" (6:13). Aliwapa changamoto na nafasi ya wao kuwa karibu naye, kumfuata na kuwa wenzi wake wa karibu. Aliwaita "Mitume" (6:13). Kutoka mwanzo aliwajulisha kwamba watakuwa watumwa wake. Aliwachagua kumi na wawili peke yake, ambao walikuwa tofauti sana. Yesu aliweka tumaini la huduma yake katika maisha ya watu kumi na wawili ambao hawakuwa na mafunzo, umahiri, na uwezo, bali walikuwa na tumaini kwamba kumfuata kutawatayarisha kubadilisha ulimwengu. Ukichukua kundi la vijana, wasiokomaa na bila mafunzo kama walivyo, na kuwachagua kuwa pamoja nawe haitawabadilisha tu, lakini muda si muda , watafanya sehemu yao kubadilisha ulimwengu.

**Husisha**. Uanafunzi uliendelea Yesu ***alipojihusisha*** na wanafunzi aliowachagua. Walipata mafunzo si kwa kuhudhuria semina au kwa kujiandikisha katika darasa, bali Yesu aliwafunza kwa kukaa nao (Marko 3:14). Mtalaa ulihusu muda waliotumia naye Yesu, wakiwa na uhusiano wa karibu kwa uaminifu kuhusika naye. Yesu aliwaambia wanafunzi wake "njooni kwangu" na "Mkajifunze kwangu" (Mathayo 11:28-30). Nao walifanya hivyo. Yale waliyoyashuhudia yaliwashangaza – maji kuwa divai, watu 5000 kulishwa, mawimbi kukomeshwa. Kukaa kwao na Yesu, kuliwawezesha kuona imani katika matendo. Kwa kujihusisha naye, walijifunza kumuamini Mungu. Kwa kujihusisha nawe, kundi ambalo umechagua litajifunza kumuamini Mungu watakapoona imani yako katika matendo.

**Weka wakfu**. Watu wengi walimfuata Yesu. Kama vile Luka anavyosema, walikuwa, "wanaandamana pamoja na Yesu" (Luka 14:25). Walipendelea kuona miujiza, kuuona umaarufu wa Yesu ukienea, na kufurahia kufaulu kwake. Lakini Yesu **aliuchuja** umati huo kwa ***kuwaweka wakfu*** wanafunzi wake wale kumi na wawili peke yao. Katika kitabu cha Luka 14:25-34, tunaona Yesu akiweka tofauti kati ya wale waliokuwa wakijionea tu na wanafunzi waaminifu. Yesu aliwapa wanafunzi wake changamoto ya kumuweka yeye mbele ya uhusiano wao mwingine wote (14:26), wamdhamini mbele ya tamaa zao zote za kibinafsi (14:27) na wawe tayari kuteseka na kujitolea ili wamfuate (14:27).

Baadaye alisimulia hadithi ambayo iliwapa nafasi ya kufikiria juu ya kuhesabu gharama. Ndipo akamalizia, ". . . hakuna hata mmoja wenu atakayekuwa mwanafunzi wangu kama asipokiachilia kila kitu alicho nacho" (14:33). Wengi wao waliondoka. Wale kumi na wawili ndio waliobaki. Tabia hii ya kuwekwa wakfu ndiyo iliyowafanya wanafunzi wa Yesu kuwa "chumvi" (14:34) iliyo na ladha katika ulimwengu mkavu. Kwa wakati unaofaa katika utaratibu, uanafunzi unamaanisha kuwaongoza hao wanafunzi kumweka Yesu mbele ya uhusiano mwingine wote, shughuli za shule, tamaa na hata maisha yenyewe. Na hapo ndipo wanafunzi wetu watajitenga na jinsi wanavyoishi na kunena. Wanafunzi wengine watatamani kuonja chumvi hiyo.

**Pasha**. Yesu alipokuwa akijihusisha na wanafunzi wake, alikuwa ***akipasha uhai*** ndani mwao. Alifanya hivyo katika kila sehemu ya maisha. Hakuandaa darasa au mafundisho ambapo alisema, "leo tunajifunza juu ya maombi". Badala yake, wanafunzi walivutiwa na mtindo wa Yesu wa kuomba mpaka wakamwuliza kwa hamu awafundishe kuomba (Luka 11:1-4). Wanafunzi wa Yesu waliendelea kupokea kutoka kwake. Walipata msimamo, mwelekeo, kuelewa, taswira na ukweli na bila kusahau maisha ya milele – maisha waliyoyapata ndani yake (Yohana 1:4, 6:35). Uanafunzi utapata ukweli watakapotuona tukiishi maisha – mazuri au mabaya na yasiyotamanika – na ndani yake wakiona maisha ya Yesu yaking'aa kutoka kwetu.

**Upendo**. Ukiondoa ***upendo*** kutoka kwa uhusiano wa Yesu na wanafunzi wake, utakuwa umeondoa sehemu muhimu sana. Yesu aliwapenda wanafunzi wake. Hakuongea tu juu ya upendo aliokuwa nao kwao, lakini alionyesha kwa njia tofauti zisizo za kawaida. Yohana akikumbuka shida zile kubwa walizokuwa nazo katika maisha yao na Yesu, je, huwa anakumbuka nini? Jinsi Yesu "aliwaonyesha upendo wake" (Yohana 13:1). Kitambulisho cha wanafunzi wa Yesu ni upendo – upendo kwa Yesu na kupendana wao kwa wao. Yesu aliwaonyeshaje, upendo huo? Katika Yohana 13, aliwatumikia kwa kuchukua nafasi ya chini kabisa ya kuwaosha miguu. Ilikuwa tendo la upendo wa kutumika. Wanafunzi wako watawezaje kumjua Yesu? Kwa upendo unaowaonyesha. Watajuaje upendo ni wa kweli? Kwa njia ambayo unawatumikia.

**Wakilishwa**. Yesu alikuwa na vitu vyote vilivyohitajika kufanya kazi yote peke yake. Lakini tunapata alionyesha wazi mambo hayo mbele yao. Na hapo akawaachia huduma yake ***wamwakilishe***. Hakufanya hivyo hapo mwanzo, alifanya hivyo baada ya kuwaonyesha wazi kwa matendo. Tia maanani kwamba aliwapa mamlaka ya kuiendeleza kazi yake. Alikuwa anaondoka. Walikuwa wanaachwa. Aliwafunza mambo yote waliyohitaji kujua. (Mathayo 10:1). Aliwapa maagizo fulani (10:5 kuf.). Aliwatayarisha kwa uadui na mateso. Aliwaahidi kwamba watapata kila kitu watakachokihitaji (10:19-20). Aliwaambia wasiogope (10:26). Aliwapa taswira kwamba mbinguni ndiyo lengo lao (10:32-39). Naye Yesu akasema watu wengine watawakaribisha (10:40-42). Unapoendelea na uanafunzi, wakati utafika na utajisikia ni wakati wa kuwapa wanafunzi wako madaraka. Wakati huo utaweza kwa busara kufuata maagizo ya Yesu kwa wanafunzi wake yaliyo katika Mathayo 10.

**Ombea**. Mara nyingi, Yesu alikuwa ***akiwaombea*** wanafunzi wake. Hata kama alikuwa anawaombea hapo awali, ni katika Yohana 17 peke yake ambapo aliomba kwa bayana na kwa upendo mwingi.

Akifikiria juu ya msalaba, na wanafunzi wake wakiwa na mahangaiko, maombi ya Yesu yaliwapa msaada ambao uliwainua katika uwepo wa Mungu wakati huu wa dharura. Pia, katika maombi yake, Yesu aliomba kwamba wawe na wema wa muda mrefu. Alimwomba Baba yake “awaweke salama” (17:11-12), awape “furaha”(17:13), na awaweke “wakfu” (17:17-19). Kuwaweka salama, furaha na wakfu. Hili ni ombi la nguvu sana likielekezwa kwa watu ambao tunawafanyia uanafunzi. Omba bayana na kwa mara nyingi.

**Tathmini**. Jambo mojawapo la muhimu ambalo Yesu alikuwa akilifanya pamoja na wanafunzi wake ni ***kuwatathmini*.** Tathmini za Yesu zilikuwa za wakati wa kufaa, na za uaminifu zilizotolewa ili kuwaongoza wanafunzi wake. Aliwasaidia kutambua “upofu wao” kama vifungu vya upumbavu vilivyo katika (Luka 10:17-20), mawazo yao yasio ya kweli (Yohana 13:36-38) na lengo lisilo la Kibiblia (Marko 10:35-45). Aliwakemea (Luka 9:51-56, Marko 8:31-33). Alijibu maswali (Mathayo 18:21-35, Mathayo 19:23-26 na mifano mingine mingi.) Katika uanafunzi, wanafunzi watanufaika kutokana na tathmini ambazo wanakundi watazitoa. Kila mmoja wetu hupoteza mwelekeo. “Upofu wetu” hutufanya tukose bila kutambua. Kuwatathmini wanafunzi wako kutawafanya kukua katika mfano wa Kristo.

**Zalisha**. Yesu alijua kwamba uanafunzi haukuwa mwisho wa yote. Ilikuwa njia ya kuelekea mwisho wa ***kuzaa matunda***. Yesu alipokuwa akianza huduma yake aliwapa motisha wanafunzi wake kuwa “wavuvi wa watu” (Marko 1:17). Baadaye, aliwafunza “kuwafanya watu kuwa wanafunzi” (Mathayo 28:18-20). Yale Yesu aliyoyafanya pamoja na wanafunzi wake, ndiyo yaliyofuatwa na kanisa la kwanza. “Kuzaa Kiroho” ndiyo iliyobadilisha ulimwengu juu chini. Kufanya uanafunzi kama vile Yesu alivyofanya huelekeza wanafunzi kuwafanyia wanafunzi wachanga uanafunzi. Kwa muda mfupi huduma yako itakuwa na kufikia kilele.

Yale Yesu aliyoyafanya na wanafunzi wake yalikuwa ya kiutendaji na halisi. Tukifanyia wanafunzi wetu uanafunzi kama vile Yesu alivyofanya, wataacha kuwa tu wahudhuriaji wa kanisa na kuwa wanafunzi ambao maisha yao yamebadilika na kuandaliwa kuwa wabadilishi wa maisha. Baadaye wataleta mabadiliko katika ulimwengu kwa ajili ya Kristo.

# MASWALI MAGUMU

Tafakari maswali haya. Jiweke katika kiwango cha 1-10. Angalia jinsi umejibu maswali hayo. Andika aya fupi ukieleza haja ya kuwafuasa vijana katika hali na mazingira yako.

1. Kuna ugumu wa kiasi gani kuwapa wanafunzi motisha ya kufuatilia mambo ya kiroho?

   1 2 3 4 5 6 7 8 9 10

2. Ni asilimia ngapi ya wanafunzi wako hujiondoa katika huduma ya vijana kuanzia kidato cha kwanza hadi cha nne? (Fanya utafiti).

   1 2 3 4 5 6 7 8 9 10

3. Ni asilimia ngapi ya wanafunzi wanaohitimu mwaka huu ambao wana roho ya kufuatilia mambo ya Mungu na kumwishia?

   1 2 3 4 5 6 7 8 9 10

4. Ni asilimia ngapi ya wanafunzi wako ambao wana shauku juu ya uhusiano wao na Mungu?

   1 2 3 4 5 6 7 8 9 10

5. Ni asilimia ngapi ya wanafunzi wako ambao wanahusika katika kundi la uanafunzi?

   1 2 3 4 5 6 7 8 9 10

6. Ni asilimia ngapi ya wanafunzi wako ambao wanahusika katika kuwafuatilia wanafunzi wachanga?

   1 2 3 4 5 6 7 8 9 10

Haja yangu ya kuwafuasa vijana na dhamani yake

# KANUNI ZA HUDUMA YA VIJANA

**Wawezaje kufanya uanafunzi kwa wanafunzi ambao watabadilika katika maisha yao na kubadilisha maisha ya wengine?**

Maisha ya wanafunzi ambao watapitia katika huduma yako yatakuwa na tofauti gani na jinsi walivyokuwa walipoanza? Ni nini inatokea pande ya mwisho wa bomba?

## Kanuni za Uanafunzi

Soma 2 Timotheo 2:1-2 mara sita. Andika muhtasari kila wakati unaposoma. Tafuta kanuni moja ya uanafunzi kila wakati unaposoma.

*Basi, wewe mwanangu, uwe na nguvu katika neema tunayopata katika kuungana na Kristo Yesu. Chukua yale mafundisho uliyonisikia nikitangaza mbele ya mashahidi wengi, uyakabidhi kwa watu wanaoaminika, ambao wataweza kuwafundisha wengine pia*

2 Timotheo 2:1-2.

1.

2.

3.

4.

5.

6.

**Katika sentensi moja, elezea kila maana ya hoja hizi kwako wewe binafsi na kwa huduma yako kwa jumla**

1. **Kupokea**

   *Basi, wewe mwanangu, uwe na nguvu katika neema tunayopata katika kuungana na Kristo Yesu.*

2. **Uhusiano**

   *. . . wewe . . . mimi . . . (Paulo na Timotheo)*

3. **Kuakisi**

   *. . . uyakabidhi*

4. **Ukweli**

   *. . . mbele ya mashahidi wengi . . .*

5. **Kuruta**

   *. . . watu wanaoaminika . . .*

6. **Zalisha**

   *. . . wewe . . . mimi . . . watu wanaoaminika.. .wengine.*

KUELEZA UANAFUNZI

Kuwapa wanafunzi kundi ndogo, uzoefu wa uwiano ulio na nidhamu, kuwajibika na kutia moyo ili kuleta matokeo ya motisha, kukua, matendo na huduma.

# HATUA ZA UTENDAJI

1. **Omba**

Uliza Mungu akuonyeshe ni nani utakayefanya uanafunzi naye na jinsi ya kufanya uanafunzi. Omba kwa ajili ya viongozi wengine wa uanafunzi ambao wamehitimu. Omba, ili wanafunzi waweze kuitikia wito. Omba Mungu awape wanafunzi wako motisha, kukua, matendo na roho ya huduma katika maisha yao.

2. **Ota**

Kutafanyika nini wanafunzi uliowafundisha wakibadilika na kuwasaidia wengine kubadilika? Kanisa na chuo chao kitaathirika kwa njia gani?

3. **Chagua**

Kutana kibinafsi na wanafunzi ambao wako tayari kwa uanafunzi. Toa maono yako. Wape changamoto ana kwa ana. Weka kiwango chako juu kwa kupitia "Ahadi za Kibinafsi" katika ukurasa 11 wa *Kumfuata Yesu (Following Jesus)*.

4. **Kujitolea**

Eleza "Ahadi za Kibinafsi" (ukurasa 11 wa *Kumfuata Yesu*) kwa wale watakaohudhuria mkutano maalum utakaouita. Wape changamoto kwa kuwaeleza kuwa itawagharimu wakati na uwaonyeshe pia kuwa ni lazima wabadilishe mambo yale wanayoyapatia kipaumbele katika maisha yao. Waonyeshe jinsi mazoea haya ni ya manufaa katika maisha yao ya Kikristo, ukuaji wa kibinafsi, umahiri wa uongozi na mvuto katika mahali pa kukusanyikia.

5. **Jitayarishe**

Kamilisha kila sehemu katika kitabu chako mwenyewe. *Mwongozo kwa Viongozi* utakusaidia kujibu maswali ya jinsi ya kuongoza kundi lako. Angalia *Mwongozo kwa Viongozi* ili upate maswali muhimu ya kuuliza wanafunzi wako, na uweze kuzungumzia mada ya siku hiyo kwa ukamilifu. Andika maswali katika kijitabu ili uweze kutumia mtakapokutana katika kundi. Usitumie *Mwongozo kwa Viongozi* wakati wa mkutano. Hakikisha umejitayarisha kabla ya mkutano!

6. **Ongoza**

Wewe ni kiongozi. Patia wanakundi hatua ya kufuata! Uliza Mungu akufanye uwe kiongozi mwema kwa wanafunzi ambao Kristo anang'aa ndani mwao. Wakitatanika wape usaidizi, wape motisha, wapigie simu, kutana nao, na mbele ya yote waombee. Uongozi wako utawaathiri sana katika maisha yao yote.

7. **Kabidhi**

Uanafunzi ni zaidi ya kukutanika kama kundi. Ni kukabidhiana kwa uwiano. Kwa kuongoza kundi hili unakuwa rafiki na mshauri. Jitolee kwa wanafunzi wako wakati hamna mkutano.


8. **Tathmini**

Kila juma baada ya mkutano wenu wa kundi, tathmini mambo yale mliyoyafanya na jinsi mnaweza kufanya vizuri zaidi. Tatua matatizo na ufanye marekebisho. Tumia vifaa vilivyo katika *Mwongozo kwa Viongozi* ili vikusaidie kutathmini.

Ili kuzidisha haya makundi ya uanafunzi, itakubidi ukiongoze kikundi chako kisha ukigawe kikundi chako cha uongozi katika makundi mawili na baadaye uyape changamoto ya kufuata mbinu au mtindo huu ili kuanzisha vikundi vyao. Muda si muda kila mwanafunzi atapata nafasi ya kufuaswa

Njia bora zaidi ya kutimiza Wito Mkuu si kupitia kwa tukio lakini ni kupitia kwa utaratibu – utaratibu wa kuwafuasa wanafunzi."




Agiza kutoka kwa tuvuti www.reach-out.org



# MPANGO WA UTENDAJI

**Kwa sasa**, ...wafanya nini ili kuwafuasa wanafunzi?

**Kupiga hatua,** ... Chukua yale umegundua na uunde mpango wa utendaji ili kuyashika na kuyafwata maono ya *Huduma ya Vijana Inayomlenga Yesu*.

**Kwa nini** ni muhimu wewe, watu wako waliojitolea na wazazi kuwafuasa vijana?

**Ni nini** utakachokifanya ili kuwafuasa vijana?

**Ni nani** vijana utakaowafuasa, na ni viongozi wapi watakaowafuasa vijana wengine?

**Ni wapi** utakapokutania na kikundi chako cha viongozi wa kuwafuasa vijana?

**Ni lini** utakapoanza na kuendelea kukutana na viongozi wako wa kuwafuasa vijana?

# Kuipenya Desturi / Tamaduni

## Lengo

Kuwaandaa na kuwakusanya viongozi, wazazi na wanafunzi ili waweze kumleta Yesu katika desturi ya wanafunzi na vijana kwa jumla.

Sehemu ya sita

# KUMTAZAMA YESU

Mara nyingi Yesu aliwapa wanafunzi hatua ya kwanza. Hakuna mahali pengine ambapo tunaona Yesu akiwa na bidii kama vile alivyokuwa wakati alikuwa akitafuta uhusiano na "wenye dhambi". Yesu alisema, "Kwa maana Mwana wa adamu amekuja kuwatafuta na kuokoa waliopotea" (Luka 19:10).

Ili tuweze kuona jinsi sisi, kama viongozi wa vijana, tunavyoweza kuwapa vijana hatua ya kwanza, katika kuwa na uhusiano na wenye dhambi, tazama mkuki. Alipokuwa pamoja na wanafunzi wake, Yesu alikuwa ncha ya mkuki, nao wanafunzi walikuwa wano. Wano hufuata ncha. Yesu alisema, "Nifuateni, nami nitawafanya kuwa wavuvi wa watu" (Mathayo 4:19). Katika huduma zetu, Mungu ametuita tumfuate Yesu na tuwe wavuvi wa vijana na tuwafanye na kuwaandaa ili nao pia wawe wavuvi wa wengine. Watafuata mfano wetu, kama vile wano hufuata ncha ya mkuki.

Marko 1-10 inatupa mifano kumi na saba ya jinsi Yesu alitupa hatua ya kwanza ya kupenya katika desturi ya wasio waamini.

- *1:14 – Yesu alikwenda Galilaya, akahubiri Habari Njema ya Mungu.*
- *1:21 – Yesu akaingia katika Sinagogi, akaanza kufundisha.*
- *1:38 – Yesu akawaambia, "Twendeni katika miji mingine ya jirani nikahubiri huko pia."*
- *2:1-2 - . . . Yesu alikuwa akiwahubiria ujumbe wake.*
- *2:13 – Yesu alikwenda tena kando ya ziwa. Umati wa watu ukamwendea, naye akaanza kuwafundisha.*
- *3:1 – Yesu aliingia tena katika Sinagogi na mle ndani mlikuwa na mtu aliyekuwa na mkono uliopooza.*
- *4:35 – Jioni, siku hiyo hiyo, Yesu aliwaambia wanafunzi wake, "Tuvuke ziwa, twende ng'ambo."*

- *6:6b – Kisha Yesu alivitembelea vijiji vya pale karibu akiwafundisha watu.*
- *6:56 – Kila mahali Yesu alipokwenda, katika vijiji, miji au mashambani, watu waliwaleta na kuwaweka wagonjwa uwanjani, . . . Nao wote waliomgusa walipona.*
- *7:24 – Yesu aliondoka hapo, akaenda wilaya ya Tiro.*
- *7:31 – Kisha Yesu alipoondoka wilaya ya Tiro, akapita Sidoni . . .*
- *8:22[a] – Yesu alifika Bethsaida pamoja na wanafunzi wake. Huko watu wakamletea kipofu mmoja, wakamwomba amguse.*
- *8:27 – Kisha Yesu na wanafunzi wake walikwenda katika vijiji vya Kaisarea, Filipi.*
- *10:1[a] – Yesu alitoka hapo akaenda mkoani Yudea, hata ng'ambo ya mto Yordani.*
- *10:17 – Yesu alipoanza tena safari yake, mtu mmoja alimjia mbio, akapiga magoti mbele yake.*
- *10:32[a] – Basi, walikuwa njiani kwenda Yerusalemu, na Yesu alikuwa anawatangulia . . .*
- *10:46[a] – basi, wakafika Yeriko, naye Yesu alipokuwa anatoka katika mji huo akiwa na wanafunzi wake pamoja na umati mkubwa wa watu, kipofu mwombaji mwana wa Timayo aitwaye Bartimayo* alikuwa ameketi kando ya barabara.

Huduma ya Yesu inatupa utambuzi wa mambo aliyoyafanya ili kupenya desturi na pia yale aliyotaka tufanye. Alieleza ombi lake wazi mara nyingi kwa kueleza Wito Mkuu katika Injili zote nne na katika Matendo (Mathayo 28:18-20, Marko 16:15, Luka 24:46-47, Yohana 20:21, Matendo 1:8). Katika Mathayo 28:18-19, alitoa maagizo kwetu: "Kwa sababu mnaenda . . ." Kwa viongozi wa vijana, anasema, "kwa sababu mnaenda, nendeni basi mahali ambapo vijana wako . . ." Kwa wanafunzi anasema, "Kwa sababu mnaenda shuleni, nendeni basi mkawafikie marafiki zenu."

***Ujumbe wake Yesu Kristo ni wa wazi na rahisi sana: Enenda na***
***Habari Njema!!!***

# MASWALI MAGUMU

Tafakari maswali haya. Jiweke katika kiwango cha 1-10. Angalia jinsi umejibu maswali hayo. Andika aya fupi ukieleza haja ya kuupenya utamaduni wa vijana mahali unapoishi.

1. Je, una uhuru kiasi kipi wa kutembea katika chuo/shule?

   1 2 3 4 5 6 7 8 9 10

2. Je unajipa kiwango kipi cha muda ambao unatumia katika chuo/shule?

   1 2 3 4 5 6 7 8 9 10

3. Kati ya wanafunzi unaowajua kwa majina, ni wangapi kati yao ambao si waamini?

   1 2 3 4 5 6 7 8 9 10

4. Ni asilimia ngapi ya watu waliojitolea ambao wanafanya huduma ya vyuo?

   1 2 3 4 5 6 7 8 9 10

5. Mafundisho unayoyatoa kwa wanafunzi ili kuwasaidia waweze kufikia wengine unaweza sema ni ya kiwango gani?

   1 2 3 4 5 6 7 8 9 10

6. Ni asilimia ngapi ya wanafunzi wanaojiona kuwa wanachama hai na wanaathiri wanafunzi wengine wa chuo/shule kiroho?

   1 2 3 4 5 6 7 8 9 10

Kujihoji kwangu kikamilifu na kikweli kuhusu haja yangu ya kuipenya desturi ya vijana mahali ninapoishi.

# KANUNI ZA HUDUMA YA VIJANA

**Wawezaje kuwatayarisha na kuwaandaa viongozi, wazazi na wanafunzi ili waweze kumleta Yesu katika desturi ya wanafunzi / vijana?**

Ni jambo la busara kwenda mahali wanafunzi walipo. Asilimia themanini na nane ya wanafunzi hawamjui Yesu. Tunajua hivyo, lakini ni watu wachache tu kanisani ambao wanachukua hatua ya kuwafikia. Jambo ambalo litatupa motisha ya kuondoka "kutoka kwa viti vyetu na kwenda barabarani" ni wakati Yesu atatubadilisha na kuwa watu wenye huruma ambao wanampenda Mungu na pia vijana. Ndipo tutalazimika kwenda. Mungu anaweza kutumia mambo gani ili kutupa motisha ya kwenda?

## Upendo wa Mungu Hutupa Motisha (Marko 6:34)

Yesu aliwaonea watu huruma. Katika Marko 6:34 tunaona kwamba Yesu, "akawaonea huruma, kwa sababu walikuwa kama kondoo wasio na mchungaji". "Huruma" ya Yesu ilimleta kwetu. Kwa njia hiyo hiyo, Mungu anataka kuzidisha "kiwango cha huruma yetu" na kutuleta karibu na vijana ambao wanamhitaji Yesu. Ametuita kushughulika katika ulimwengu ambao watu hawajishughulishi.

## Yesu Ametuita Kutoka Katika Sehemu Zetu za Starehe (Yohana 20:21)

Yesu alitoka mahali pake pa starehe. Fikiria Yesu akiwa katika mkono wa kulia wa Mungu, akifanya uamuzi wa kuja katika tumbo la uzazi, azaliwe kama mwanadamu, alazwe katika hori la ng'ombe, afungwe katika mwili wa mwanadamu, apate lengelenge za viatu, avumilie jasho, vumbi, na chakula kibaya. Aliacha starehe za kuwa kando ya Baba yake ili avumilie hayo! Alifanya uamuzi huo mgumu na ametuita tufanye vivyo hivyo.

> Huruma ni njia ya kuonyesha kwamba tunajali katika ulimwengu usiojali.

## Ili Kuwafikia Vijana, Lazima Tuende Mahali Walipo (Yohana 1:14)

Yesu "akakaa" kati yetu. Alikuja mahali tulipo ili baadaye twende mahali alipo. Kwa sababu tunamfuata Yesu, tunatakiwa twende mahali vijana walipo ili baadaye waje mahali tulipo.

## Vijana Huwa na Uchungu Usiosadikika (Luka 5:12-16)

Yesu aliuhisi uchungu kama ulivyo. Aliuhisi uchungu aliokuwa nao mtu yule mwenye ukoma. Na hakuona aibu kwa sababu yake. Badala yake, aliugusa. Kizazi hiki kina uchungu zaidi ya kizazi kingine cho chote katika historia. Wao ni kama mtu aliyekuwa na ukoma, aliyekuwa na tamaa ya kutaka kuponywa. Wanahitaji mponyaji ambaye ana majeraha (Isaya 53:4-6). Yeye tu ndiye tumaini lao. Sisi, kama Kristo tunatoa uponyaji kwa vijana walio na uchungu mwingi.

## Wanafunzi / Vijana Wahitaji Kujua Kwamba kuna Yule Ambaye Anawajali (Luka 15:1-2)

Yesu alichagua kimaksudi kukaa na wenye dhambi. Alijua uchaguzi wake utamtenga na viongozi na waelekezi wa dini iliyokuweko. Hili halikumshtua. Kwa nini? Alikuwa amepanga mambo yake. Alikuwa anataka wenye dhambi wajue kwamba anawajali zaidi ya vile alitaka wenye dini wampende. Vijana hutaka kujua kwamba kuna mtu anayewajali. Tunapowajali vijana, watu wa dini huudhika. Hawataki watu wa "namna hiyo" ndani ya kanisa. Kuwa kama Yesu, kutatugharimu, hasa na watu wa dini. Ilimgharimu Yesu maisha yake!

## Vijana Wanamhitaji Yesu (Yohana 17:3)

Vijana wanautaka uhai. Lakini hawajui waupate wapi. Tunajua mahali pa kuupata. Unapatikana ndani ya Yesu na si mahali pengine po-pote. Yesu alisema, "Na uhai wa milele ndio huu: kukujua wewe uliye peke yako Mungu wa kweli, na kumjua Yesu Kristo uliyemtuma" (Yohana 17:3). Kwa wazi kabisa, wanafunzi wanaweza kuupata uhai ndani Yake Kristo– kupitia kwetu sisi.

**Vijana wataweza kuyapata maisha ndani mwake Kristo kupitia kwako!!**

## Yesu Amewatangulia (Mathayo 28:7, 10)

Yesu alifufuka, na kama vile malaika alisema, "Na sasa anawatangulieni kule Galilaya" (Mathayo 28:7). Yesu aliyefufuka hatutumi katika desturi ya wanafunzi peke yetu, ametutangulia na tutampata huko. Yesu anaendelea kufanya kazi ndani ya maisha ya wanafunzi. Anatungojea tuungane naye huko!

Agano jipya lina nyakati mara mbili – *Chronos* na *kairos*. *Chronos* ni kupita kwa wakati wa kila siku. Ambao unafanyika kwa watu wote kila siku. Lakini *Kairos* ni wakati maalum wa kihistoria. Yesu aliishi wakati wa *kairo*s kwa miaka mitatu akiwa katika hali ya kibinadamu: "Lakini wakati ule maalum (kairos) ulipotimia. . ." (Wagalatia 4:4). Tunapoishi ndani yake katika hali yake ya kiroho, huwa tunaishi katika wakati maalum (kairos). Kuna wanafunzi kati yetu ambao wanamhitaji Yesu na ambao hawatampata isipokuwa watujue. Katika wakati huu wa kairos, Mungu anatuongoza tuweze kupitia vizuizi vyote ili tuwafikie wanafunzi hawa katika desturi zao. Huu ndio wakati!

> Pengine changamoto kuu ya kanisa wakati huu ni kuwafikia wale walio nje ya kanisa, kuita kizazi kichanga kumfuata Yesu.

# HATUA ZA UTENDAJI

Enda kando ya njia ya miguu ilyoko katikati ya shule au chuo kilicho karibu nawe. Fika wakati wanafunzi wanatoka shuleni au wanaelekea shuleni kisha ujiulize kwamba ni wangapi wa vijana hawa wanamjua Kristo kibinafsi. Yale utakayoyashuhudia yatakutia motisha wa kutaka kuwafikia vijana kwa dharura.

Basi wazia na kukusudia kuchukua hatua zifuatazo katika shule au mji ulio karibu nawe.

## Kupenya Ndani ya Chuo/Shule/Kikundi

Ukiwa na mzigo kwa wanafunzi ndani ya roho yako, unahitaji kuchukua hatua gani ili uweze kuwafikia?

1. **Omba kukubalika (Matendo 2:47)**

   Rudia sehemu ya maombi na uchukue hatua unazozihitaji ili kutimiza mkakati wa kuomba kwa shauku ambao utakuhusu wewe, watu watakaojitolea, wazazi na wanafunzi. Lenga maombi yako kwa shule moja. Uliza Mungu akufanye kukubalika katika shule hiyo. Tumia ***Jinsi ya Ajabu ya Kuomba*** (*Awesome way to pray*) kama chombo cha kukuongoza katika maombi.

2. **Jenga Daraja – Jifahamishe na Shule (Matendo 17:16)**

   Ili kufahamu shule, unahitaji kufuata hatua zinazoweza kutumika.
   - Soma gazeti au ripoti ya mwaka ya shule hiyo.
   - Hoji watoto wako. Waulize maswali juu ya shule yao.
   - Jiunge na wanafunzi wakati wa matukio yao na kuwa na wakati nao. Andika muhtasari.
   - Soma "Kukagua Shule" katika ***Kupenya chuo***.

3. **Vuka daraja – Ongea na Mwalimu mkuu (Waefeso 6:7)**

   Ili uweze kuvuka daraja kwenda kwa mwalimu mkuu wa shule, ni lazima ufanye uamuzi muhimu.

   *Nitasimamia haki zangu za kibinadamu katika shule hii*

   ***Au** nitanyenyekea kwa shule na kuwatumikia?*

   Njia ya pekee ya kuwa na uhusiano wa muda mrefu na uongozi wa shule hiyo ni kwa kuwatumikia. Ukifanya uamuzi wa kuwatumika kama vile Yesu alivyotumika, basi njia ya kuwa na uhusiano na mwalimu mkuu inafunguka.

Fuata hatua hizi unapojenga uhusiano:

- Msikutane kiofisi. Tafuta mzazi wa mwanafunzi wako aweze kukujulisha kwa mwalimu mkuu wakati wa sherehe moja katika shule hiyo.
- Baada ya kukutana, mwandikie mwalimu mkuu barua.
- Sasa fanya ahadi mkutane ki rasmi katika ofisi yake.

- 4. Baadaye, mwandikie mwalimu mkuu barua ya kumshukuru tena.
- Endela kuimarisha uhusiano kwa kukutana naye mara kwa mara.

4. **Weka Daraja Wazi – Kuwa Mtumishi Katika Shule (Yohana 13:1-17, Wakolosai 3:23-24).**

Ili uweze kupata mahali ambapo Mungu anataka utumike katika shule hiyo:

- Tafuta sehemu unayopenda kutumika au hitaji walilo nalo.
- Ongea na wanafunzi na walimu ili uweze kujua mahitaji yao.
- Kama hauna uhakika, jaribu mambo tofauti. Tumia wakati wako ukisaidia.

5. **Kuwa na Uhusiano na wanafunzi (Yohana 4:1-2**)

Soma kwa makini mfano wa mazungumzo ya Yesu katika Yohana 4 uweze kutambua jinsi Yesu alivyoanza urafiki na mtu ambaye hawakufahamikiana naye.

- Uliza maswali na usikize. Uliza: nani, nini, wapi, lini, kwa nini na kwa jinsi gani? Waweza kuongea na mtu ye yote kwa karibu dakika 15 ukiuliza maswali hayo.
- Chukua hitaji moja, kutoka katika mahitaji hayo, mpe tumaini.

6. **Waandae watu wa kujitolea (Wakolosai 4:7-15)**

Yesu alikuwa na wanafunzi kumi na wawili. Paulo alikuwa na wanafunzi wengi. Wengine wametajwa katika Wakolosai 4:7-15. Tazama jinsi Paulo anavyotaja kazi tofauti wanazozifanya.


Waweza kuwaandaa watu waliojitolea.


- Tafuta njia ya kulihusisha kundi lako la viongozi, ukijua kwamba wana muda mfupi sana.
- Tafu njia ya kulinganisha uwezo mbali mbali wa viongozi wako na mahitaji ya shule.
- Wasaidie kulenga kundi moja la wanafunzi kwa masaa machache kwa juma.
- Wasaidie wazazi kuwa na uhusiano na marafiki za watoto wao kwa kuwaalika katika nyumba zao na kuwaandalia chakula.
- Watafute na uwahusishe wanafunzi wa chuo/shule na wale wasio na wenzao, ambao wana wakati mwingi wa kujitolea.
- Unda kikundi katika chuo/shule mkiwa pamoja na viongozi wa watu waliojitolea.
- Ungana na viongozi wengine Wakristo wa chuo/shule hiyo.

7. **Andaa wanafunzi (Mathayo 10, Matendo 8:1-4)**

Tena, jione wewe na viongozi wako na wazazi kama ncha ya mshale na wanafunzi kama wano. Kazi yako ni kuwapa hatua ya kufuata, waandae na uwape changamoto ya kupelekea marafiki zao Kristo.

**Agiza kutoka kwa tuvuti: [www.reach-out.org](http://www.reach-out.org)**



MPANGO WA UTENDAJI WA KUIPENDA DESTURI / TAMADUNI

# MPANGO WA UTENDAJI

**Kwa sasa**, ...wafanya nini ili kuupenya utamaduni / desturi?

**Kupiga hatua,** ... Chukua yale umegundua na uunde mpango wa utendaji ili kuyashika na kuyafwata maono ya Huduma ya Vijana Inayomlenga Yesu.

**Kwa nini** ni muhimu wewe naviongozi wako kuupenya utamaduni / desturi?

**Ni nini** utakachokifanya ili kuupenya utamaduni / desturi?

**Ni nani** haswa ambao umekusudia kuwafikia?

**Ni wapi** utakapoupenya utamaduni / desturi?

**Ni lini** utakapoupenya utamaduni / desturi?

# Buni Nafasi za Kuwafikia Wengine

## Lengo

Kuzieleza Habari za Yesu kupitia nafasi zinazohusu desturi ya wanafunzi inayokubalika ili wanafunzi wawalete marafiki zao wasioamini kwa Yesu

**Sehemu ya saba**

**Buni Nafasi**
**za Kuwafikia Wengine**

7

## KUMTAZAMA YESU

**Yesu alijua jinsi ya kujitambulisha. Yohana aliandika**;

> Siku ya mwisho ya sikukuu hiyo ilikuwa siku maalum. Yesu alisimama akasema kwa sauti kubwa, “Aliye na kiu na aje kwangu anywe. Kama yasemavyo Maandiko Matakatifu: `Aniaminiye mimi, mito ya maji ya uhai itatiririka kutoka moyoni mwake!’”
>
> Yohana 7:37-39

Mwalimu wetu mkuu: Bwana Yesu Kristo anatuonyesha jinsi ya kuzieleza habari zake kupitia nafasi zinazohusu desturi ya vijana ili nao wawalete marafiki zao wasioamini kwake.

Sikukuu ya vibanda ilikuwa siku maalum ya ukumbusho kwamba wana wa Israeli walikuwa wanazurura jangwani mahali ambapo maji yalikuwa kitu cha dhamani na gumu kupata. Wakati wa sherehe hiyo kuhani alichukua gudulia la dhahabu, na kuliteremsha katika bwawa la Siloamu na kulijaza maji. Aliyabeba maji, na kuingilia mlango maalum uliotumika wakati wa sherehe hii – Mlango wa Maji – nao wakati huo huo, watu walikuwa wakikariri Isaya 12:3, “Mtachota maji kwa furaha kutoka kwa visima vya wokovu.”Alibeba maji hayo hekaluni na kuyamwaga juu ya madhabahu kama sadaka kwa Mungu.

Inawezekana wakati huo, maneno ya Yesu yalikuwa, “Aliye na kiu na aje kwangu anywe.” Kila mmoja alipata ujumbe. Yesu alisema, yeye ni maji ya uzima yaliyoashiriwa katika sherehe hii. Kulikuwa na joto jingi na vumbi, naye akawaalika waje ili mahitaji yao yaweze kutimizwa – wapate kunywa maji. Baadaye alitoa agizo kwamba kila amwaminiye atapata mito ya maji ya uzima ambayo itatiririka kutoka mioyoni mwao. Changamoto kubwa kwa viongozi wa vijana ni kumtambulisha Yesu kama vile alivyojitambulisha - Kwa ujasiri na kuwaadhiri wanafunzi ili kumuelewa Yesu kuwa ni nani, ili watamani kunywa kutoka kwake na kubuni nafasi za kumtambulisha Yesu kwa njia ambayo wanafunzi watatamani maji hayo ya uzima.

## Kupitia Nafasi za Uinjilisti zinazohusu Desturi Inayokubalika

Lawi alijua jinsi ya kumtambulisha Yesu kwa njia iliyokubalika kwao. Ulikuwa muda mfupi baada ya yeye kukutana na Yesu (Luka 5:27-28). Hilo ni dokezo! Njia bora ya kuwashuhudia wanafunzi waliopotea ni kupitia kwa wanafunzi waliookoka hivi majuzi. Wakati, kama vile Lawi, “ameacha kila kitu na kumfuata” atakuwa na hamu kubwa ya marafiki wake kufanya vivyo hivyo.

Lawi, alitaka marafiki wake kumjua Yesu kama vile Luka anavyotuonyesha katika kifungu cha 5:29: “Lawi akamwandalia Yesu karamu kubwa nyumbani mwake. Na kundi kubwa la watoza ushuru na watu wengine (wenye dhambi) walikuwa wameketi pamoja nao.” Lawi aliandaa karamu. Aliandaa karamu ili aweze kusherehekea maisha mapya aliyokuwa ameyapata ndani ya Yesu.

Weka maanani kwamba, Lawi aliandaa mazingira ambayo yalikubalika kwakeYesu na kwao marafiki zake Lawi vilevile. Wanafunzi Wakristo wanahitaji kupata nafasi ya kuwaleta marafiki zao wasio Wakristo kwa Yesu. Na wanafunzi wasio Wakristo wanahitaji kuwa huru Yesu akiwa kati yao. Shida nyingi ambazo huduma nyingi za vijana huwa nazo ni kuandaa mazingira ya pande mbili zitakazokubalika kwa wahusika wote wawili.

## Ambapo Watu Wataleta Marafiki zao wasio Wakristo

Wanafunzi wake Yesu walikuwa wamepoteza mwelekeo wa jinsi ya kuwaleta wenye dhambi kwa Yesu. Katika kitabu cha Marko 10:13, walitaka kuwazuia watoto waliokuwa na sauti kubwa na wasiostaarabika kwenda kwa Yesu. Watu walimletea Yesu watoto wadogo ili awaguse, lakini wanafunzi wakawakemea. Mara nyingi watu wa kanisa na watu walio na ushawishi mwingi katika kanisa ndio “hukemea” – huleta vizuizi ambavyo huzuia wenye dhambi, kwa tabia na matendo yao, lugha, nyimbo fulani au michezo isiyofaa.

Tazama aliyoyafanya Yesu ili kuigeuza hali hiyo.

> Yesu alipoona hivyo, alikasirika akawaambia, “waacheni hao watoto waje kwangu, wala msiwazuie, kwa maana ufalme wa Mungu ni kwa ajili ya watu walio kama watoto hawa. Nawaambieni kweli, mtu yeyote asiyeupokea ufalme wa Mungu kama mtoto mdogo hataingia humo.” Kisha akawapokea watoto hao, akawawekea mikono, akawabariki
>
> *Marko 10:14-16*

Kama vile wanafunzi walivyofanya, ni rahisi kuyabainisha makundi ya vijana kulingana na utamaduni, rangi, umri, muziki wanaousikiza, tabia, mavazi, na vitendo vyao. Tunapofanya hivyo, huwa tunawazuia wengine kupata Injili. Mara nyingi tunapobuni nafasi za kufanya uinjilisti, huwa tunabuni tukiwa na maoni hayo. Baadaye tunashangaa ni kwa nini wenye dhambi hawaji au wanakuja na hawampokei Kristo. Kama wawakilishi wa Yesu, Roho wake akiwa ndani mwetu, ni lazima tuondoe vizuizi na kutengeneza njia kupitia kwa nafasi za uinjilisti ili wanafunzi Wakristo waweze kuwaleta wasioamini kwa Yesu.

*Katika utamaduni wetu, nimegundua kwamba watoto ambao hawaendi kanisani – wengi wao wanahusika katika mambo ambayo yanahatarisha maisha yao na wana bidii ya kidini. . . lakini, kundi letu la vijana wadogo hujiweka mahali pa salama . . .*

*Leo hii, vijana wanahitaji kuyahatarisha maisha yao kwa ajili ya kumfuata Kristo. Wengi wao wanangoja kanisa liwape jambo kubwa, jambo la maana au jambo la kuthubutu ili walifanye.*

*PAUL BORTHWICK*

## MASWALI MAGUMU

Tafakari maswali haya. Jiweke katika kiwango cha 1-10. Angalia jinsi umejibu maswali hayo. Andika aya fupi ukieleza haja ya kuzibuni nafasi za kuwafikia wengine hata kupitia kwa utamaduni unaokubalika

1. Je, unajipa kiwango kipi katika kumfikia kila kijana katika kila chuo/kijiji katika jamii yako?

1 2 3 4 5 6 7 8 9 10

2. Je, unajipa kiwango kipi katika kufaulu kwako kuwaeleza vijana juu ya Kristo wewe binafsi?

1 2 3 4 5 6 7 8 9 10

3. Ni asilimia ngapi ya vijana walio wanafunzi wako wana mawazo ya huduma na umishenari?

1 2 3 4 5 6 7 8 9 10

4. Unapoenda kufanya uinjilisti, huwa na kiasi gani cha urafiki na wasiookoka?

1 2 3 4 5 6 7 8 9 10

6. Huwa na asilimia ngapi ya wasiookoka katika tukio la uinjilisti?

1 2 3 4 5 6 7 8 9 10

7. Ni asilia ngapi ya wanafunzi/vijana wako walimpokea Yesu mwaka uliopita?

1 2 3 4 5 6 7 8 9 10

# KANUNI ZA HUDUMA YA VIJANA

Kwa njia gani huwa tunamtambulisha Yesu kwa kueneza habari zake kupitia nafasi zinazohusu desturi au utamaduni unaokubalika ambapo watu huwaleta marafiki zao wasioamini kwa Yesu.

## Tabia Nne

Tunapotazama Agano Jipya tunaona jinsi Yesu alivyobuni nafasi za kufanya uinjilisti, tabia nne zinajitokeza.

1. **Yesu ndiye aliyeangaziwa (Marko 1:40-45).**
   Ingawa mwenye ukoma aliponywa na muujiza kutendeka, Yesu ndiye aliyekuwa shujaa kiasi kwamba watu wengi walitoka sehemu mbalimbali kuja kumuona.

2. **Umati ulijawa na shauku (Marko 4:1 ).**
   Umati ulijawa na shauku hata ukajazana na kumsukuma Yesu hadi ukingo wa maji hata ikambidi kuingia kwenye jahazi.

3. **Waumini walitaka marafiki zao wasio waamini wakutane na Yesu (Luka 5:27-29).**
   Lau, mtoza ushuru aliyedharauliwa alikutana na Yesu. Kwa shauku kuu alitaka rafiki zake wakutane naye na akawaandalia karamu.

4. **Mioyo ilibadilishwa milele (Mathayo 20:29-34).**
   Vipofu wawili walipolia kwa sauti wakiomba rehema, Yesu kwa huruma aligusa macho yao waliponywa na wakamfuata Yesu- wamebadilishwa milele.

# Mitazamo Miwili

Ili uweze kuwa na ushawishi mkuu katika maisha ya vijana, tazama taswira hizi kama vile unazitazama kupitia kwa darubini iliyo na lenzi mbili.

**Mtazamo wa 1 – Lenga Yesu**

Wasaidie vijana kumjua Yesu. Kijana mmoja akimpokea Yesu huwa ni jambo linalofaa. Ni rahisi kupoteza mwelekeo huu ukidhania kuwa ni ukubwa wa tukio ndio unaojalisha. Kufaulu hakutegemei idadi, bali katika kuwasaidia vijana kumpokea Kristo.

**Mtazamo wa 2: Elewa Kusudi**

Ukiwa na kusudi, hautajiuliza "nitawaburudisha na nini sasa?" Kwa kila nafasi ya uinjilisti andika kusudi la nafasi hiyo.

# Nafasi Tano za Kuchagua

Unapojiandaa na hata baada ya kukamilisha kuwafikia watu , utapata kwamba umetumia mda mwingi wa mahusiano. Ili kuzuia kuutumia mda mrefu sana, tafiti nafasi zako mapema kisha uchague itakayo chukua mda mchache lakini iliyo bora.

Nafasi yoyote utakayoichagua, hakikisha kwamba umewahusisha wanakikundi chako cha uanafunzi.unaweza kuwapa majukumu ya kubuni nafasi za kuwafikia watu au uwape majukumu kwa ajili ya mikutano mikubwa ya uinjilisti. Kwa vyovyote vile, wanafunzi hujichukulia mikutano hiyo kuwa yao na wakakuza vipaji vya uongozi wao. Wao huchukuwa majukumu ya kuwaandaa na kuwaleta marafiki zao .

1. **Kuiga mfano**

Kanuni inayofaa hapa ni “Duniani hakuna jambo jipya” (Mhubiri 1:9). Jifunze kutokana na makundi mengine ya uinjilisti. Omba vifaa vya uinjilisti kutoka kwa jumuiya. Waweza kualika wahubiri kutoka makanisa mengine wakati wa mwisho wa juma.

2. **Anzisha**

Ni vigumu kuanzisha jambo, lakini ni jambo la kuzawadiwa kupata kundi la wafanya kazi wa vijana na wanafunzi wakiwa katika chumba kimoja, kila mmoja akitoa mawazo yake ili kufanya jambo geni. Hapa tunapata kanuni mpya: “Watu huunga mkono jambo ambalo wameanzisha wenyewe.”

3. **Igharamikie**

Kuna watu binafsi au kundi la watu ambao huwa na mipango ambayo imeshaandaliwa na wako tayari kuileta katika kanisa lako kwa malipo madogo. Vijana katika vyuo huwa na mashirika ambayo yana makundi ya wanafunzi ambao wako tayari kuja na kufanya uinjilisti kikamilifu. Hakikisha umetembelea kundi hilo kabla ya kuwaalika ama umepata hakikisho kutoka kwa viongozi tofauti wa vijana ambao wamekwisha watumia.

4. **Jiunge**

Kuwa mwangalifu ili uweze kujua mahali ambapo kuna maonyesho ya muziki, mashindano ya mpira na nafasi zingine katika sehemu ambazo waweza kutumia kufikia lengo lako la uinjilisti. Hii inakusaidia kuepuka shida zote za utaratibu na mzozo wa usafirishaji wa watu na vitu ambavyo huambatana na mipango ya uinjilisti. Hakikisha umefuatilia waamini wapya ili uinufaishe huduma yako.

5. **Kodisha**

Mara nyingi, ikiwezekana kodisha badala ya kununua. Viwanja vidogo vya burudani, uwanja mdogo wa gofu, bwawa la kuogelea, ukumbi wa michezo wa mazoezi ya viungo, uwanja wa michezo na vyumba vya maonyesho waweza kukodishwa ili uwe na nafasi ya kufanya uinjilisti. Kuwa mbunifu!

**Usiwahi kuwachosha vijana Kwa injili** ***Jim Rayburn***

# HATUA ZA UTENDAJI

## Panga Bata Wako Katika Mstari

Ili kuleta ubunifu katika mpango wa uinjilisti, itakuwa vyema ukitumia “njia ya kuandika hadithi kwa ubao”. Ukitumia njia hii kwa kila uinjilisti, utagundua mawazo na matendo yako uliyoyabuni na uyafanye mapya katika kila uinjilisti. Andika wazo ulilobuni na lililokufaa katika kila uinjilisti katika ukaratasi au kwenye kitabu chini ya aina zifuatazo:

1. Kusudi: Kusudi moja la nafasi hii ya uinjilisti ni gani?
2. Wakusudiwa: Ni nani hasa mnayemkusudia?
3. Dhamira: Dhamira bayana ni gani?
4. Lengo: Lengo lako bayana ni lipi?
5. Wazo: Ni mawazo yapi bunifu katika mpango huu? (Panga pamoja na timu yako ya viongozi au wanafunzi wako. Baada ya kuandika chini mawazo yote ya kundi ambayo yanahusu dhamira na lengo, chagua mawazo matano ambayo yanawafaa zaidi?)
6. Rasilimali: Ni rasilimali gani hasa inayohitajika?
7. Matokeo: Mpango utakuwaje? Ni nani atahusika na atahusika wapi?  Na Lini?

## Ongoza Bata Wako Kuelekea Upande Mmoja


Ili kuwaelekeza viongozi, wazazi na vijana wako katika njia moja, hakikisha unafuata kusudi na lengo la uinjilisti. Weka kifungu kilichoandikwa lengo la uinjilisti katika ukuta wa chumba ambamo mnafanyia mipango.

Kwa maombi, ufuate mpangilio wako wakuwafikia watu na kikundi chako hadi mumefaulu. Waweza kuomba ombi hili:

***Bwana twahitaji kumuwasilisha Yesu kwa njia ya kiutamaduni/desturi za vijana zinazokubalikana zitakazowaleta vijana wasiokujua kukujua. Amen.***

Kumbuka lengo la Mungu:

Kumfikia kila kijana na ujumbe wa Yesu unaobadilisha maisha!




**Agiza kutoka tuvuti www.reach-out.org.**

## MPANGO WA UTENDAJI

**Kwa sasa**, ...wafanya nini ili kubuni nafasi za kuwafikia wengine?

**Kupiga hatua,** ... Chukua yale umegundua na uunde mpango wa utendaji ili kuya shika na kuyafwata maono ya Huduma ya Vijana Inayomlenga Yesu.

**Kwa nini** ni muhimu wewe na viongozi wako kubuni nafasi za kuwafikia wengine?

**Ni nini** utakachokifanya ili kubuni nafasi za kuwafikia wengine?

**Ni nani** haswa vijana hao wasioamini, ambao wanafunzi wako wanaweza kuwaalika kwa kikao chao kitakachofuata cha kuwafikia wengine?

**Ni wapi** utakapoandaa mkutano wa kuwafikia wengine?

**Ni lini** utakapoandaa mkutano mwinginewa kuwafikia wengine?

# Kuyaweka yote Pamoja

## Lengo

Kuugundua mpango wa utendaji wa kipekee wa Mungu kwa ajili ya huduma yako ya vijana inayomlenga Yesu

Kuyaweka yote Pamoja

## *Wawezaje kuuweka pamoja mpango wote wa Huduma ya Vijana Inayomlenga Yesu?*

Ukitafakari kuhusu yale umeyagundua katika Huduma ya Vijana Inayomlenga Yesu, unahitaji kufanya nini ili uweze kusonga kutoka utangulizi (kujifunza Kanuni hizi) mpaka utekelezaji (kutumia kanuni hizi katika hali yako)?

Weka muda wako kando, inafaa sana kama ni masaa matatu yanayofuatana, ili uweze kutafakari juu ya vifaa hivi na hasa kurasa za mpango wa utekelezaji. Uchukulie kama "wakati wa kimya na kutafakari kwa muda kibinafsi ili upate maono." Ondoka kutoka shughuli zingine zote na uwe na wakati wako pekee na Mungu. Weka pamoja mipango yako yote ya utekelezaji katika kurasa zifuatazo ili uweze kuwa na mpango wako wote wa huduma ya vijana.

Kurasa za muhtasari wa mpango wa utendaji na zile zipatikanazo katika kila sehemu zimeongezewa ili uzitumie kwa njia itakayo kufaa zaidi.

## Muhtasari wa Mpango wa Utendaji

Tumia Muhtasari wa mpango wa utendaji unaopatikana katika ukurasa unaofuata kuiweka mipango yako yote ya utendaji katika ukurasa mmoja. Unapo rejelea kila sehemu, tafuta wazo moja na matendo matatu ya kufuata.

- Fanya muhtasari wa mpango wa utendaji wako kuwa sehemu ya maombi yako ya kila siku kwa ajili ya huduma yako.
- Tumia muhtasari wa mpango wa utendaji wako kuandika maono ya huduma yako kisha uyakabidhi kwa mchungaji wako na viongozi.

Nakala mbili za muhtasari wa mpango wa utendaji wako zimejumuishwa.

## Kurasa za Muhtasari wa Mpango wa Utendaji

Tumia Kurasa za muhtasari wa mpango wa utendaji kama nafasi za kufanyia kazi na kuundia mipango yako ya huduma ya vijana inayomlenga Yesu. Kurasa hizi zitakufaa utakapoyatathmini malengo yako ya mwakani.

# MUHTASARI WA MIPANGO YA UTENDAJI

| | |
|---|---|
| | **Kuwa na Uhusiano wenye Kina na Kristo** |
| Utambuzi muhimu zaidi | Hatua za utekelezaji<br>1.<br>2.<br>3 |
| | **Kuomba kwa shauku** |
| Utambuzi muhimu zaidi | Hatua za utekelezaji<br>1.<br>2.<br>3 |
| | **Kuwaandaa viongozi** |
| Utambuzi muhimu zaidi | Hatua za utekelezaji<br>1.<br>2.<br>3 |
| | **Kuwafuasa wanafunzi** |
| Utambuzi muhimu zaidi | Hatua za utekelezaji<br>1.<br>2.<br>3 |
| | **Kupenya desturi** |
| Utambuzi muhimu zaidi | Hatua za utekelezaji<br>1.<br>2.<br>3 |
| | **Kubuni nafasi za kuwafikia wengine** |
| Utambuzi muhimu zaidi | Hatua za utekelezaji<br>1.<br>2.<br>3 |

# MUHTASARI WA MIPANGO YA UTENDAJI

| | **Kuwa na Uhusiano wenye Kina na Kristo** |
|---|---|
| Utambuzi muhimu zaidi | Hatua za utekelezaji<br>1.<br>2.<br>3 |
| | **Kuomba kwa shauku** |
| Utambuzi muhimu zaidi | Hatua za utekelezaji<br>1.<br>2.<br>3 |
| | **Kuwaandaa viongozi** |
| Utambuzi muhimu zaidi | Hatua za utekelezaji<br>1.<br>2.<br>3 |
| | **Kuwafuasa wanafunzi** |
| Utambuzi muhimu zaidi | Hatua za utekelezaji<br>1.<br>2.<br>3 |
| | **Kupenya desturi** |
| Utambuzi muhimu zaidi | Hatua za utekelezaji<br>1.<br>2.<br>3 |
| | **Kubuni nafasi za kuwafikia wengine** |
| Utambuzi muhimu zaidi | Hatua za utekelezaji<br>1.<br>2.<br>3 |

***MHUTASARI WA MPANGO WA UTENDAJI WA***

## ...KUWA NA UHUSIANO WENYE KINA NA

**Kwa sasa**, ...wafanya nini ili kuwa na uhusiano wenye kina na Kristo?

**Kwenda mbele,** ... Chukua yale umegundua na uunde mpango wa utendaji ili kuyashika na kuyafwata maono ya Huduma ya Vijana Inayomlenga Yesu.

**Kwa nini** ni muhimu wewe kuwa na uhusiano wenye kina na Kristo?

**Ni nini** utakachokifanya wewe ili kuwa na uhusiano wenye kina na Kristo?

**Ni nani** utakayewajibika kwake ili uwe na uhusiano wenye kina na Kristo?

**Ni wapi** utakapokutania na Kristo ili uwe na uhusiano wenye kina naye?

**Ni lini** na wakati upi utakaoutenga ili uwe na wakati mwema wa kuhusiano kwa kina na Kristo?

***MHUTASARI WA MPANGO WA UTENDAJI WA***

## ...KUOMBA KWA SHAUKU

**Kwa sasa**, ...wafanya nini ili kuomba kwa shauku

**Kupiga hatua,** ... Chukua yale umegundua na uunde mpango wa utendaji ili kuyashika na kuyafwata maono ya Huduma ya Vijana Inayomlenga Yesu.

**Kwa nini** ni muhimu wewe nawenzako katika huduma yako kuomba kwa shauku?

**Ni nini** mtakachokifanya wewe na wenzako katika huduma yako ili muombe kwa shauku?

**Ni nani** atakayejiunga nanyi katika kikundi chenyu cha watatu, na ni nani katika huduma yako atakaye anzisha vikundi vingine vya watatu watatu?

**Ni wapi** kikundi chenyu cha watatu kitakapokuwa kikikutania kwa kuomba?

**Ni lini** kikundi chenyu cha watatu kitakuwa kikikutana kwa maombi?

***MHUTASARI WA MPANGO WA UTENDAJI WA***

## ...KUWAANDAA VIONGOZI

**Kwa sasa**, ...wafanya nini ili kuwaandaa viongozi?

**Kupiga hatua,** ... Chukua yale umegundua na uunde mpango wa utendaji ili kuyashika na kuyafwata maono ya Huduma ya Vijana Inayomlenga Yesu.

**Kwa nini** ni muhimu kwaandaa viongozi?

**Ni nini** utakachokifanya ili kuwaandaa viongozi?

**Ni nani** hao viongozi utakaowaandaa?

**Ni wapi** utakapokutania na kikundi chako cha viongozi?

**Ni lini** utakapoanza na kuendelea kukutana na kikundi cha ko cha viongozi?

***MHUTASARI WA MPANGO WA UTENDAJI WA***

...UANAFUNZI

**Kwa sasa**, ...wafanya nini ili kuwafuasa wanafunzi?

**Kupiga hatua,** ... Chukua yale umegundua na uunde mpango wa utendaji ili kuyashika na kuyafwata maono ya Huduma ya Vijana Inayomlenga Yesu.

**Kwa nini** ni muhimu wewe, watu wako waliojitolea na wazazi kuwafuasa vijana?

**Ni nini** utakachokifanya ili kuwafuasa vijana?

**Ni nani** vijana utakaowafuasa na ni viongozi wapi watakaowafuasa vijana wengine?

**Ni wapi** utakapokutania na kikundi chako cha viongozi wa kuwafuasa vijana?

**Ni lini** utakapoanza na kuendelea kukutana na viongozi wako wa kuwafuasa vijana?

***MHUTASARI WA MPANGO WA UTENDAJI WA***

## ...KUIPENYA DESTURI/UTAMADUNI

**Kwa sasa**, ...wafanya nini ili kuupenya utamaduni / desturi?

**Kupiga hatua,** ... Chukua yale umegundua na uunde mpango wa utendaji ili kuyashika na kuyafwata maono ya Huduma ya Vijana Inayomlenga Yesu.

**Kwa nini** ni muhimu wewe naviongozi wako kuupenya utamaduni / desturi?

**Ni nini** utakachokifanya ili kuupenya utamaduni / desturi?

**Ni nani** haswa ambao umekusudia kuwafikia?

**Ni wapi** utakapoupenya utamaduni / desturi?

**Ni lini** utakapoupenya utamaduni / desturi?

***MHUTASARI WA MPANGO WA UTENDAJI WA***

## ...BUNI NAFASI ZA KUWAFIKIA WENGINE

**Kwa sasa**, ...wafanya nini ili kubuni nafasi za kuwafikia wengine?

**Kupiga hatua,** ... Chukua yale umegundua na uunde mpango wa utendaji ili kuyashika na kuyafwata maono ya Huduma ya Vijana Inayomlenga Yesu.

**Kwa nini** ni muhimu wewe na viongozi wako kubuni nafasi za kuwafikia wengine?

**Ni nini** utakachokifanya ili kubuni nafasi za kuwafikia wengine?

**Ni nani** haswa vijana hao wasioamini, ambao wanafunzi wako wanaweza kuwaalika kwa kikao chao kitakachofuata cha kuwafikia wengine?

**Ni wapi** utakapoandaa mkutano wa kuwafikia wengine?

**Ni lini** utakapoandaa mkutano mwinginewa kuwafikia wengine?

# Maswali Yanayoulizwa Kwa Wingi

# Maswali Yanayoulizwa Kwa Wingi juu ya Huduma Ya Vijana Inayomlenga Yesu

Maswali yote katika sehemu hii yanajibu mambo muhimu unayokumbana nayo katika maisha na huduma. Majibu haya ya kina yanaweza kupatikana katika kurasa za raslimali katika sehemu zote. Unaweza kuagiza na utumie raslimali zaidi.

Agiza kwenye tuvuti: www.reach-out.org

**KUWA NA UHUSIANO WENYE KINA NA KRISTO**

1. **Nitajuaje nimesamehewa?**

Kukosa msamaha huzuia kutiririka kwa upendo wa Mungu na uhai ndani yetu. Mara nyingi ni vigumu kupokea msamaha. Lakini Mungu anatoa msamaha bure. Yesu alikuwa na ujasiri alipomwambia mtu aliyekuwa amepooza kwamba dhambi zake zimesamehewa. Ili kuonyesha alikuwa na uwezo wa kusamehe dhambi, Yesu alimponya (Marko 2:1-13). Mungu aliweka agano hili: "Lakini tukiziungama dhambi zetu, basi, Mungu ni mwaminifu na mwadilifu, naye atatusamehe dhambi zetu na kututakasa uovu wote" (1 Yohana 1:9). Kwa hivyo, ukihitaji msamaha, ungama dhambi zako, na zitashughulikiwa na lile Yesu alilolifanya wakati alilipia dhambi zako juu ya msalaba. Mara nyingi, shida yetu ni kwamba huwa tunapambana sana na kujisamehe. Tunaungama dhambi zetu lakini tunashikilia hatia. Wakati Yesu alikufa, alikufa si kwa ajili ya dhambi zetu tu bali alikufa pia kwa ajili ya hatia zetu. Achilia dhambi na hatia zako ili, "kama mashariki ilivyo mbali na magharibi, ndivyo azitengavyo dhambi zetu mbali nasi" (Zaburi 103:12).

2. **Nawezaje kuomba msamaha, na ninawezaje kumsamehe mtu mwingine?**

Kuomba msamaha. Mambo mengi yamesemwa katika Biblia kuhusu kuwasamehe wengine kama tu vile yamesemwa kuhusu msamaha wa Mungu kwetu. Bila kutoa msamaha na kupokea msamaha, tutazuia si tu uhusiano wetu na Mungu lakini pia uhusiano wetu na wengine. Ili kuomba msamaha kutoka kwa mtu mwingine, fuata maagizo ya Yesu yaliyo katika Mathayo 5:23-24.

- Kumbuka kwamba ndugu yako ana ugomvi nawe. Omba Mungu na atakuonyesha yule mtu ambaye hauna uhusiano mwema naye.

- Patana. Katika hali ya unyenyekevu na kutubu, mwendee mwenzako na umuombe msamaha. Ni jambo muhimu kuweza kueleza ombi lako la kutaka msamaha vyema. Si vyema kusema "Samahani" au "Kama nimekosea. . ." Badala yake, eleza bayana makosa yako. Baadaye sema, "Waweza kunisamehe?" Hiyo inampa mtu huyo mwingine jambo thabiti la kukujibu.

Kutoa msamaha. Kumsamehe mtu ambaye amekukosea, fuata maagizo ya Yesu katika Mathayo 7:3-5 na 18:15-18. Mtu akikusononesha, hakikisha umefanya maafikiano na kuvunjwa moyo, hasira, na uchungu ulio ndani yako kwanza. Omba Mungu aondoe "boriti lililoko jichoni mwako" kwa kutoa msamaha kwa mtu huyo mwingine. Ili uweze kufanya hivyo, weka kiti upande mwingine wa kiti chako, fikiria kuwa mtu huyo ameketi kwenye kiti hicho. Mwambie juu ya kusononeka kwako. Msamehe kwa kusema, "Nimekusamehe kwa .................." Utakapoenda kwa mtu huyo kunena juu ya jambo hilo, waweza kwenda huku upendo wa Kristo ukitiririka ndani yako, kwa sababu jambo hilo tayari limesuluhishwa ndani ya roho yako.

3. **Nawezaje kubadili mwenendo mbaya katika maisha yangu?**

Hatuwezi kujibadilisha; ni Mungu ambaye hutubadilisha. Kwa nini ni vigumu sana kwetu kujifunza haya? Wagalatia 2:20-21 hutuongoza tunapokabiliana na mambo haya. Kifungu cha 21 hutuonyesha mambo yale tunayohitaji kufanya ili tuweze kubadili mienendo – "tunakataa neema ya Mungu" kwa sababu tunafikiri tunaweza kuzishughulikia hali zetu sisi wenyewe. Lakini tunapofanya hayo huwa tunamwambia Mungu: "Kristo alikufa bure." Ufunguo wa kubadili mwenendo ni "neema ya Mungu."Ambayo imeelezwa kama, "Uwepo wa Kiungu ambao uko ndani yako kwa njia ya msalaba na ufufuo." Kwa kweli Wagalatia 2:20 inatumika hapa. Ili tuweze kubadili mienendo yetu tunahitaji kukubali kweli hizi mbili muhimu:

- Wakati Kristo alikufa, nilikufa. – "Mimi nimesulubishwa pamoja na Kristo msalabani."
- Yesu alipofufuka, nilifufuka. Kupitia kwa ufufuo wa Yesu kutoka kwa wafu na kuachiliwa kwa Roho Mtakatifu, na sasa naishi lakini si mimi tena, bali "Kristo anaishi ndani mwangu."

Tuna rasilimali za Mungu zinazoishi ndani mwetu. Hivyo basi, tuishije maisha yetu? "Kwa imani katika Mwana wa Mungu." Tunaweka imani yetu katika ahadi ya Mungu: Nimekufa kwa hivyo siwezi kubadilisha kitu chochote. Lakini Kristo anaishi ndani yangu, kwa hivyo anaweza kubadilisha kila kitu. Yesu hutufanya kuwa "wenye haki" (kuwa na uhusiano sawa naye) ili tuweze kuenenda "sawa"!

**4. Na jee, kama siwezi tatua shida muhimu katika maisha yangu?**

Wakati mwingine, watu huwa na shida ambazo "hutawala maisha yao" (*Life Dominating Problems)* ambazo zimetoka kutoka kizazi kimoja hadi kingine. Kwa dhambi ambazo zimekita mizizi kama hizi, utahitaji mtu mwingine wa kukusaidia kujua jinsi ya kutumia uwepo wa Kristo. Ili kumpata mtu atakayekufaa:

- Kumbuka kwamba Roho Mtakatifu ndiye mshauri mkuu (Yohana 14:15-18).
- Muombe Mungu akupe mtu wa kukushauri ambaye anafaa.
- Tafuta mshauri mwenye msimamo thabiti ndani ya Kristo, si mwenye saikolojia ya kibinadamu. Kuna hata washauri wengine "Wakristo" ambao hawana ushauri ambao msingi wake ni Kristo
- Omba Mungu akuhuishe, akuponye na akuweke huru (Yohana 8:32,36).

5. **Nawezaje kumjua Mungu vyema zaidi?**

Kuwa na uhusiano wa karibu na Kristo ndilo lengo letu. Maisha yetu ya kiroho hutiririka kutoka kwa maji ya uzima (Yohana 4:13). Yale yote tunayoyatenda hujitokeza kutokana na hali yetu. Kwa ajili ya hayo, ni lazima tumlenge Yesu na nafsi yake iliyo ndani yetu. Tabia na mazoea yetu yatatusaidia kukua zaidi katika upendo wa Kristo.

- Jizoeshe "kupumua kiroho." Kama vile sisi huwa tunavuta na kutoa pumzi ili tuishi kimwili, tunapumua kiroho kwa kutubu dhambi zetu (kutoa pumzi), kulingana na ahadi iliyoko katika 1Yohana 1:9, na kuachilia Roho Mtakatifu ndani yetu (kuvuta pumzi), kulingana na Waefeso 5:18. Kufanya hivyo kila siku kutatufanye tukae na uhai wa kiroho.
- Omba ukitumia Maandiko unayoyakariri.
- Kuwa na wakati wa kimya na Mungu kila siku kwa dakika thalathini.
- Kariri Maandiko. Anza kwa kukariri kifungu kimoja kila juma na baadaye uongezee utakapozoea kukariri vifungu.
- Jaribu kuwa na siku nzima au nusu ya kufunga na kuomba mara moja kwa mwezi.
- Soma vitabu ambavyo vinalenga uhusiano wako na Kristo, hasa vya kujifunza maombi. Hakikisha umebeba kitabu kila wakati, na ujiwekee kiwango cha idadi ya kurasa utakazosoma kila siku.

# KUWAANDAA VIONGOZI

1. **Nawezaje kuwapata/kuwasajili/kuwakurutu viongozi wenye sifa njema?**

Watu wengi wa kawaida hujiona hawafai kuongoza, hasa huduma ya vijana. Mara nyingi huogopa. Unapowasajili viongozi, ni vyema uweze kuwaondolea uoga wao. Wajulishe kwamba hututafuti watu ambao wana mafunzo na ujuzi wa kufanya kazi na watoto, bali unatafuta watu ambao wanaweza kuwa viongozi na wana hamu ya kujifunza. Unatafuta watu ambao ni waaminifu, wana nafasi na wana hamu ya kujifunza. Unaenda kuwaandaa kwa ajili ya huduma ya vijana. Njia bora ya kuwapata ni kumwendea kila mmoja kibinafsi. Waambie, "Nataka kuanzisha kundi la viongozi wa huduma ya vijana. Tutakutanika kila juma ili tuweze kukua pamoja katika uhusiano wetu na Kristo, na uhusiano wa sisi kwa sisi, kujifunza jinsi ya kuhudumia mahitaji ya watoto kama vile Yesu alivyofanya. Waweza kuomba kwa ajili ya kujiunga nami?" Tia mkazo kwamba huu si mkutano wa kuongea juu ya mpango wa vijana, lakini ni wakati wa nguvu nyingi kuwasaidia wakue na wahudumu. Warudie baada ya siku chache ili upate majibu yao.

2. **Nahitaji viongozi wangu wote wakomavu wahusike katika kundi la viongozi?**

Si kwa mara ya kwanza. Unapoanza utakuwa ukitafuta watu ambao wana motisha, wale ambao wana hamu ya kujiunga. Wataanzisha mazingira kwa ajili ya huduma yote. Kikundi chako cha viongozi kikiwa na watu ambao hawana motisha, watapunguza kiwango cha shauku cha wanakundi wengine. Hii itapenyeza katika huduma yote. Lakini ukiwa na watu ambao wana motisha, watawawekea watoto mwongozo wa kutamanika. Utakapokuwa ukitafuta kundi lingine la viongozi, pia utataka kupata viongozi ambao wana motisha. Baada ya muda usiokuwa mrefu, viongozi wako wote watakuwa wamepata mafundisho na wana motisha. Ukifikia hapo, itamlazimu kila kiongozi atake kujiunga na kikundi cha viongozi.

3. **Naweza kuwaongeza watu wapya baada ya kuanzisha kikundi cha viongozi?**

Ukitangazia kanisa kuhusu kundi la viongozi na uwe na kikao cha kufikiria juu ya maono na/au mkutano wa kwanza, si rahisi mtu mwingine kutaka kujiunga baada ya kundi kuanza. Watu wengine wakitaka kujiunga na kundi la viongozi baada ya kuona shauku iliyoko katika kundi, waulize waweze kungoja mpaka mwisho wa majuma ya kwanza 12. Wakati huo, waweza kuchukua kundi lingine na muweze kupitia ***Kutembea na Yesu Kibinafsi*** *(A Personal Walk With Jesus)*, kitabu cha kwanza katika kifaa cha "kuwaandaa viongozi." Waweza kufanya hivyo mara nyingi iwezekanavyo ili uweze kuwa na viongozi wengi. Kundi la viongozi likiongezeka, waweza kukutana nao katika vikundi

vidogo. Ni vyema wakutane wote pamoja katika kundi kubwa kwa muda mfupi ili waweze kupata matangazo na mambo ya kuendeleza kundi, baadaye waende katika makundi madogo ya timu ya viongozi. Funza viongozi waliokomaa kuongoza makundi mapya. Njia nyingine ni kukutana na kila kundi la viongozi wakati tofauti tofauti katika juma.

4. **Nifanyeje ikiwa mtu hataendelea kushikilia kujitolea kwake kuwa katika kundi la viongozi mpaka mwisho?**

Njia ya kupunguza shida kama hizi ni kuhakikisha umefanya kazi njema kwa kukuruta/kuwasajili watu kibinafsi, kuendesha mkutano wa kueleza maono vyema, na kueleza kikamilifu "Kujitolea kibinafsi" ulio katika ukurasa wa 11 katika vitabu vyote vitatu vya vifaa vya "kuwaandaa viongozi". Kama kuna mmoja wa wana kundi ambaye ana matatizo yo yote ya kutumia vifaa hivyo au kama kundi lote lina matatizo, msifiche. Waulize shida zao nje ya kundi. Mara nyingi kuna watu ambao wana matatizo katika maisha yao ya kibinafsi ambayo yamewafanya kukosa mwelekeo au shauku. Wasaidie kutatua matatizo yao. Pengine kuna wale ambao wana utaratibu wa kufanya mambo ya kiroho. Wasaidie kugundua jinsi mambo yalivyo na jinsi ya kufanya mambo kwa njia inayofaa. Pengine alijiunga na kundi baadaye akagundua kwamba hapendi kufanya kazi na vijana. Mruhusu atoke. Mara nyingi, watu wasipotekeleza kazi waliyopewa, hawana shida na kazi. Shida huwa ni ya kibinafsi. Kama kiongozi, ni wajibu wako kuwasaidia kutatua shida zao. Kujihusisha kwako katika maisha yao kutawasaidia "kuruka viunzi" ili waweze kuendelea.

5**. Mtu akijitokeza ambaye hafanyi kazi vyema na watoto nitafanya nini?**

Kama mtu ameitwa katika huduma ya vijana, na ajitokeze, mtafutie mahali ambapo anaweza kuhudumu. Akiwa katika kundi la viongozi, utapata nafasi ya kumchunguza mwito wake, karama zake za kiroho, umahiri na uwezo wake wa kufanya kazi na wengine. Mtafutie mahali ambapo anaweza kusaidia kulingana na uwezo wake. Kuna uwezekano kwamba mtu huyo amewekwa mahali asipostahili. Pengine anafunza shule ya Jumapili na jambo lile analopenda kufanya ni utoaji wa video. Mweke mahali ambapo anaweza kutumia umahiri wake kwa njia inayofaa. Kama shida yake ni mtazamo wake, hili ni jambo tofauti. Wakati mwingine watu watajaribu kukuchezea au kukutawala kwa werevu. Kwa kisa kama hicho, ongea na kanisa lako, na uweze kukabiliana naye ana kwa ana kulingana na Biblia. Kama mtu huyo hawezani kabisa na watoto, kwa upole mwongoze aweze kuhusika katika sehemu nyingine kanisani isipokuwa huduma ya vijana. Kwa jumla, kazi yako ni kumsaidia mtu huyo aweze kupata mahali pake katika mwili wa Kristo.

# UANAFUNZI

1. **Nani anayefaa kuliongoza kundi la wanafunzi?**

Jinsi utakavyojibu swali hili kutaathiri motisha na kina cha huduma yako kwa vijana wako. Jibu kwa uangalifu ukiweka maanani iliyo ya kipekee katika hali yako.

**Kwanza**, jua kwamba wale watu walio katika timu ya viongozi ndio watakaoongoza makundi. Hiyo inaleta maana kwa sababu viongozi wako wana nafasi ya kuwa katika "kundi la uanafunzi" kila juma katika mkutano wa timu ya viongozi. Wao ndio wanaoweza kujua jinsi ya kuandaa mazingira ambayo wanafunzi wanaweza kukua vizuri.

**Pili**, usimlazimishe kila mtu ambaye amejiunga na timu ya viongozi kuongoza kundi la wanafunzi. Inawezekana kuwa huo si mwito wao katika huduma ya vijana. Waweza kuwatia moyo kuongoza kundi moja na upate wale ambao wanahamu na wamehitimu kuongoza.

**Tatu**, usiwe na matumaini ya juu sana. Anza kwa kundi moja au mbili – pengine kundi moja la wasichana na moja la wavulana. Ongoza kundi moja ili uweke ratiba ya timu ya viongozi ambao watafuata. Pia, itakupa muda wa kuamua jinsi ambayo utataka muundo wa huduma ya uanafunzi uhusishe vijana wengi zaidi. Tumia wakati kuchagua viongozi wako.

**Nne**, endelea kuandaa viongozi kwa ajili ya kundi lijalo la uanafunzi. Watu watakapokuwa wakipitia katika namna ya kuunda timu ya viongozi, watie moyo kufanyia vijana uanafunzi. Wape kundi na waonyeshe jinsi ya kuanza. Kwa kutumia mtazamo huu utaweza kuwa na wanafunzi wengi ambao wanakua katika Kristo na ambao wana shauku ya Kristo. Vijana ambao wameshakuwa wanafunzi watakuwa kiini chako. Baadaye watawafanya vijana wachanga wanafunzi.

2. **Nitawezaje kuwapa vijana changamoto ya kuwa katika kundi la uanafunzi?**

Unataka vijana ambao wanamtaka Kristo wajiunge na kundi la uanafunzi. Si lazima wawe wamekomaa kiroho ili waweze kujiunga na kundi hili. Itashangaza kwamba, vijana wengine ambao hauwatarajii ndio wataitikia changamoto yako. Mpokee kila mmoja wao katika hali yake; baadaye mpeleke mahali anapotakiwa kuwa. Njia ya kutoa changamoto kwa watoto ni muhimu sana.

- Toa changamoto kwa kundi lote, baadaye fuatilia kwa kuchagua watu binafsi. Vijana wengine ambao unaona wakiwa na uwezo inawezekana wasiitikie wakati unapotoa changamoto kwa kila mtu. Waendee kibinafsi na uwape changamoto yao.
- Waeleze gharama ya kujitolea kwa kupitia "Kujitolea kibinafsi" ulioko katika ukurasa wa 11 wa *Kumfuata Yesu.*
- Waeleze faida ya uanafunzi na uwape mifano ya maisha yako mwenyewe au maisha ya vijana wengine ambao wamepitia masomo ya uanafunzi.
- Katika mkutano wa kwanza na kundi lako, pitia maagano ya kujitolea (pia katika mkutano mwingine wowote wa kwanza) ili waweze kuona uzito wa ahadi hii. Uliza kila mtu

kibinafsi kama anaelewa yale yanayohusika.

- Wacha waweke sahihi katika agano la "kujitolea kibinafsi." Pitisha vitabu ili kila mmoja wao aweze kutia sahihi kwa kila kitabu cha mwenzake. Hii hujenga uajibikaji. Ikiwa kundi lako ni la watoto wadogo, ni vyema wazazi wao waweke sahahi kwa sababu watahusika pia.

3. **Nifanye nini wanafunzi wasipofanya kazi waliyopewa?**

Ukifuata hatua zinazofaa kutoa changamoto kwa wanafunzi, hautakuwa na shida nyingi (tazama swali la 2). Lakini wasipofanya kazi unayowapatia, jaribu kuwapa motisha kwa njia nyingine. Kufaulu kwa njia hizi kutategemea uhusiano wako na vijana hawa. Ni jambo la kushangaza kuwa wakati utakapokuwa nao nje ya kundi utachangia katika jinsi watakavyokuwa na motisha ya kuhusika katika kundi hili na kufanya kazi waliyopewa.

- Wapigie simu kila juma mara mbili au tatu kabla ya mkutano. Waulize hali yao na uwakumbushe juu ya kazi yao ya kufanya. Hii ni njia ya kujenga uhusiano nao, na kuwakumbusha yale unayoyatarajia.

- Wapange kwa njia ambayo, kila mmoja ana rafiki ambaye atakuwa akiwajibika kwake. Wajibu wao ni kusaidia ili waweze kufanya kazi. Mtoto ambaye ana motisha ya hali ya juu anaweza kumsaidia yule mwenye motisha ya chini.

- Ikiwa kuna mmoja ambaye ana shida ya kufanya kazi yake, kutana naye ili muweze kufanya kazi pamoja.

- Ikiwa kundi lote lina shida na kazi yao ya kufanya, zungumzeni wazi. Kuwa na uwazi ni kwa nini wana shida na kazi yao. Tafuteni jibu pamoja. Cho chote mtakachofanya kuwa pamoja nao. Usiwape wazo lolote kwamba utawaacha kwa sababu hawafanyi mazoezi ya ziada ya kufanyia nyumbani .

- Tumia mambo ambayo wanajifunza. Wanafunzi wana elimu nyingi lakini hawapati changamoto, kile wanachohitaji ni mahali pa kutekeleza yale wanayojifunza. Enda nao wanaposhuhudia mmoja wa marafiki zao au mnaweza kutembelea mahakama ya watoto nao, baada ya mkutano wenu wa juma. Cho chote mtakachofanya kisiwe cha kuimarisha wazo kwamba kumfuata Yesu ni jambo lisilovutia!

4. **Ni vyema wasichana na wavulana wawe katika kundi moja?**

Hapana, labda iwe ni lazima. Kutokana na ujuzi wa miaka mingi tumeona ni vyema kuwaweka watu wa jinsia moja pamoja. Si jambo la kisheria au amri ya zamani ambayo ilisema "watu wa jinsia tofauti wasiogelee pamoja." Biblia inatupa mwelekeo kwa kutueleza wazee wafundishe vijana na wanawake wazee waeleze wanawake vijana (Tito 2:1-8). Njia hii inafaa kwa sababu mbili za kiutendaji:

- Ukiweka wasichana na wavulana pamoja, watu wengi watajiandikisha kuwa katika

kundi la uanafunzi ili waweze kuwa na rafiki wa jinsia tofauti badala ya kutaka kumjua Yesu vyema.

- Kuna mambo ambayo hujitokeza katika kundi la uanafunzi na wanafunzi hutaka kujadiliana; kama vile ngono na kupiga punyeto. Wakiwa wote pamoja ni vigumu kujadili mambo hayo. Kundi za jinsia moja hutoa nafasi ya majadiliano ya kindani na ya uaminifu.

5. **Wanafunzi wangu wameshaa soma masomo ya msingi. Naweza kuruka vitabu vya "kukua katika kiroho"? Ni lazima nifanye vitabu kulingana na utaratibu?**

Viongozi wengi wa vijana hudhania kwamba wanafunzi wao wanajua mengi zaidi ya yale wanayojua, au kufikiria wamekomaa zaidi ya jinsi walivyokomaa. Hata kama wameshapitia vitabu vya msingi, haimaanishi kwamba wamekuwa wakitekeleza yale yote wamesoma. Ni vyema usiruke kitabu cho chote kwa sababu baadaye utawapa changamoto ya kuwafanyia wanafunzi wadogo uanafunzi. Wasipopitia vitabu hivyo hawatajua jinsi ya kuongoza kundi lao. Ni vyema zaidi kufanya vitabu kulingana na mpango kwa sababu vimeandikwa kwa utaratibu, kwa kuongoza vijana kutoka wokovu wa *Kumfuata Yesu* na kuwa na umahiri wa kuhudumia wengine katika *kuathiri ulimwengu*. Lakini, kama una jambo unalotaka kusisitiza, waweza kubadilisha orodha yake. Kwa mfano, Kama una safari ya umisheni na ungetaka kuwafundisha wanafunzi jinsi ya kushiriki imani yao, basi waweza kutumia kitabu cha *Kushiriki Imani Yako* hata kama si kitabu ambacho kinafuata kulingana na utaratibu.

# KUIPENYA DESTURI/TAMADUNI

**1. Nitafanya nini kama shule haziruhusu wageni kuingia humo?**

Duniani kote, ni vigumu kwa wageni kuingia ndani ya shule au vyuo. Ukweli ni kwamba kama unatumia njia inayostahili, hakuna shule ambayo itakukataza kuingia humo. Viongozi wengi wa vijana hutumia jambo hilo kama kisingizio cha kutohudumu shuleni. Kama maono ya huduma ya vijana yameeleweka vyema, inaeleza kwamba kuna hamu ya kuanzisha huduma katika kila chuo cha jumuiya zetu.

Kuvunja kuta za chuo ambacho kimefungwa:

- Omba na uombe tena. Hili ndilo jambo muhimu zaidi ya yote. Kwa miaka mingi, vyuo vingi ambavyo wageni walikuwa wamezuiliwa kuingia wameruhusiwa kwa sababu ya maombi. Kuomba kwa uaminifu kutaleta mabadiliko. *Reach Out Youth Solutions* yaweza kukusaidia na mikakati maalum ya maombi.
- Kutana na mkurugenzi/mwalimu mkuu ili uweze kuwa na uhusiano wa karibu naye.
- Kutana na mahitaji yao. Tazama mahali ambapo shule hii inahitaji msaada. andaa vifaa kutoka kwa huduma yako na kanisa ili muweze kutimiza hitaji hilo.
- Shirikiana na shirika lingine. Mara nyingi utapata kuwa kuna shirika la vijana ambalo linafanya kazi katika kila chuo. Na kama hakuna, basi fanya mpango wa kuanzisha moja. Hiyo itakupa nafasi ya kuhudumu katika chuo hicho usipopata nafasi ya kufanya hivyo kupitia kanisa lako.
- Kwa habari zaidi angalia maelezo yaliyotolewa juu ya *Kupenya katika Chuo*

2. **Nitawezaje kuhusisha timu yangu ya viongozi katika huduma ndani ya chuo?**

Utapata watu katika timu yako ya viongozi ambao watakuwa na msisimko wa kuhudumu ndani ya chuo/shule na wengine hutetemeka kwa uoga. Kwa njia yoyote, kila mmoja anatakiwa kujihusisha na watoto nje ya kanisa kwa njia moja au nyingine, hata kama watajitolea kwa lisaa limoja tu kila juma. Chukua wale ambao wana shauku ya huduma. Waweke chuoni mahali ambapo watajifunza mtakapokuwa mkifanya kazi pamoja. Wakishaa fundishwa , wasaidie kuanzisha huduma ndani ya chuo/shule nyingine. Msaada muhimu katika huduma chuoni ni wanafunzi wa chuo hicho. Tumia wakati walio nao na umri wao ulio karibia ule wa watoto wa shule, wapange katika makundi ya timu za chuo ili waweze kuwa na uhusiano na watoto wa kila chuo katika jumuiya yako. Sehemu nzima imetengwa ili uweze kuelewa jinsi ya *kupenya katika chuo*.

3. **Una haki gani katika chuo?**

Huna! Wanafunzi wana haki kiasi na waalimu wana haki kiasi fulani kulingana na nafasi za kuwakilisha. Kama wewe ni mzazi wa mwnafunzi, basi haki zako ni sawa na za wazazi wengine. Lakini, wewe, kama kiongozi wa vijana katika kanisa la mtaa, hauna haki zozote. Kwa sababu hilo ni jambo muhimu, kuweza kupanga njia ambayo utaingia chuoni nayo kwa kuamua kutumia "njia ya utumishi" badala ya kutumia "njia ifaayo". Badala ya kwenda chuoni na kuomba kuwe na wakati wa kujifunza Biblia, chama, au nafasi ya kuongea na wanafunzi ndani ya darasa au wakati wa mikutano yao, jenga uhusiano na mkurugenzi na waalimu na hapo uweze kuamua jinsi unavyoweza kutimiza mahitaji ya chuo hicho. Huo utakupa uhusiano mwema, na wa muda mrefu na shule hiyo na itakupa nafasi ya kuhudumia wanafunzi kwa muda wa miaka mingi.

**4. Nifanyeje kama kuna zaidi ya chuo kimoja katika sehemu yangu?**

Ni bora kuwa na vyuo vingi katika sehemu moja! Kama una vyuo vingi katika sehemu yako, huduma yako ina nafasi kubwa ya kuwafikia wanafunzi wengi zaidi. Chukulia kuwa na vyuo vingi kama jambo jema badala ya jambo lisilostahili. Ukitumia mtazamo kuwa ni jambo linalofaa, utafanya nini ili uweze kuwafikia?

- Wewe, kama kiongozi, anzisha huduma inayofaa ndani ya chuo hicho.

- Tumia chuo kama mahali pa kufundishia timu yako ya viongozi jinsi ya kufikia wanafunzi wa chuo.

- Unda timu za chuo ukitumia wanafunzi wa chuo ambao wako katika timu yako ya viongozi na ambao huona chuo kama sehemu yao ya huduma. Anzisha huduma katika chuo kingine wakati utaona kwamba una timu ya viongozi ambao wanaweza kuhudumu kikamilifu.

- Iambie timu ya chuo kuandaa wanafunzi Wakristo waweze kuwavuta marafiki zao kwa Kristo. Kitabu kwa jina "kuchukua chuo chako kwa Kristo" kitakupa vifaa unavyohitaji kutekeleza huduma hii.

- Usifikirie kuwa waweza kufikia kila chuo ukiwa peke yako au kupitia kanisa lako peke yake. Fanya kazi pamoja na mashirika mengine ya Wakristo yanayohudumu katika vyuo na makanisa mengine, ndio, hata dini zingine ili kuhakikisha kwamba kila mwanafunzi wa kila chuo katika jumuiya yako amepata nafasi ya kumjua na kumfuata Kristo.

**5. Nifanye nini, kanisa langu likinizuia kwenda chuoni?**

Ni vigumu kujibu swali hili kwa sababu kuna mambo tofauti ambayo yanaweza kumfanya mchungaji wako au viongozi wako kukuzuia kuwa na huduma ya chuo. Ukichukulia kwamba hakuna mtu anayetaka kuwa kiongozi na hakuna mapigano kati yako na viongozi, ni vyema kugundua ni kwa nini hawataki uwe na huduma ya chuo. Kuna uwezekano kwamba kuna jambo wanalolijua ambalo hulijui juu ya hali hiyo. Mungu anaweza kuwa anawatumia kwa sababu wakati ufaao haujafika. Ukigundua ni tofauti ya falsafa na maono ambayo yanahusu jambo ambalo viongozi wako hawana hamu ya kuwafikia vijana kwa ajili ya Kristo, au "kutaka kuwa na wanafunzi wa aina hiyo katika kanisa letu" basi unalo tatizo kubwa.
Ili uweze kutatua tatizo lako:

- Omba Mungu akupe hekima na mwelekeo.
- Hakikisha viongozi wako wameelewa maono yako, hata kama wanakubaliana nayo au la andika maono yako.
- Peleka ombi lako kwa viongozi wako kuhusu jambo hili. Waulize waweze kulitilia maanani.
- Tambua kwamba "wawili hawawezi tembea pamoja mpaka wakubaliane." Unaweza tafuta njia nyingine kama hawataki ufanye huduma hiyo. Kwa wakati huu, waweza kuwazia kuhamia katika huduma nyingine. Ukiwa na matumaini kwamba mkiendelea katika huduma, utaweza kuwashawishi yaliyo katika roho yako, naye Mungu atakupa uhuru wa kumfikia kila mwanafunzi katika kila shule kwa ajili ya Yesu Kristo.

## BUNI NAFASI ZA KUWAFIKIA WENGINE

1. **Ufanyeje, kama hauna kipawa, pesa au watu wa kubuni nafasi ya uinjilisti nao?**

Kama vile Yesu alivyozidisha mikate mitano na samaki wawili, ukitoa kile ulicho nacho kwa Mungu kwa imani, atakuzidishia na kubuni jambo ambalo ni zaidi ya lile unalofikiria. Ili Mungu aweze kuzidisha rasilimali yako, fuata hatua zifuatazo za utendaji:

- Omba kwa bidii.
- Fuata hatua zilizotolewa katika swali la 2 ili uweze kujitayarisha kwa nafasi ya uinjilisti.

- Kuruta watu wa kufanya kazi nawe kupitia kwa timu yako ya viongozi. Waweza kukuruta watu ambao mwelekeo wao ni kubuni nafasi za kuwafikia wengine.

- Kurata vipawa kutoka jumuiya au kutoka kanisa lingine ambao watakusaidia. Hakikisha mna lengo moja.

- Kwa ubunifu, changisha pesa kwa kuwauliza kundi la vijana kufadhili watakaochangisha pesa au kwa kuwaendea viongozi wa kanisa na kuwaomba pesa.

- Tambua pia kwamba, waweza kutumia sherehe za watu wengine kuwafikia wengine na pia waweza kuungana na makanisa mengine kuandaa sherehe.

- Haijalishi rasilimali yako, ukiomba, viongozi wa kanisa wakikuunga mkono, na umefunza viongozi wako na wanafunzi, enda kwa imani na uanze na uache Mungu atimize mahitaji yako "zaidi ya yale tuwezayo kuomba na kufikiria" (Waefeso 3:20).

2. **Ninahitaji nini ili niweze kujitayarisha kuwa na nafasi bora, bunifu za kuwafikia wengine?**
Swali hili lina umuhimu mwingi, kulijibu kulichukua kurasa za kwanza 76 za kitabu kiitwacho *Athari ya Sumaku*! Kitabu hiki kinakuonyesha jinsi ya kuandika kifungu chako cha kazi maalumu (wito) kwa ajili ya huduma yako, kuweka mkakati wa Biblia wa huduma ya vijana, kuzuia wanafunzi kupinga Injili kwa maombi, na kuhusisha viongozi wa kanisa lako, timu yako ya viongozi na kiini cha wanafunzi walio nyuma yako. Hata kama utaratibu huu utachukua muda mrefu zaidi ya vile unavyotaka, ni vyema kungojea ili uweze kufanya kwa njia inayofaa. Kumbuka hutaki kibonge cha sufi bali matunda ya muda mrefu.

3. **Nitapataje vijana wasio Wakristo kuhudhuria?**
Kanisa ambalo lengo lake ni kuwafikia vijana wasio Wakristo litashinda katika kizazi hiki. Kwa kweli kanisa ambalo halifikii vijana wasio Wakristo, wataachwa katika mavumbi. Ili kuwavutia na uweze kuwafikia ni muhimu kuwa na uhusiano nao. Hiyo ina maana kuwa kupenya ndani ya chuo ni jambo muhimu kwa kufaulu katika kuwafikia Vijana hawatavutiwa na kung'aa kwa mpango, lakini watakuja kwa sababu wamekuja na marafiki zao. Ili hayo yatendeke ni lazima ukusudie kuwafikia vijana wasio Wakristo. Hawatakuja kwa bahati. Viongozi wako na wanafunzi lazima wawe na hamu ya kulete marafiki zao. Hayo yakifanyika, vijana wasio Wakristo watakuja. Ukitarajia kwamba watakuja zaidi ya mara moja, basi itakubidi ubuni mpango ulio na upungufu wa "ukristo" na unaofaa mahitaji ya vijana wasio Wakristo. Hiyo inamaanisha kuwa na mpango bora sana. *Athari ya Sumaku* inakuelekeza katika utaratibu wa kufanya hivyo.

4**. Nahitaji kuwafikia wengine kwa kutoa Injili kila Juma?**

Anza pole pole. Anza kwa kuwa na nafasi ya kuwafikia wengine mara moja baada ya miezi mitatu. Viongozi

na wanafunzi wako wakiendelea kukomaa waweza kuandaa mara moja kwa mwezi, baada ya hapo mara moja kwa juma. Kuwa na msimamo ni jambo muhimu kwa sababu inakusaidia wewe, viongozi wako na wanafunzi wako kujua kwamba kutakuwa na nafasi ya kuwafikia wengine mara kwa mara. Lakini kutoa Injili kila Juma, jibu ni ndio. Lakini haina maana kuwa utoe ujumbe sawa wa uinjilisti kila juma. Kwa kutumia ubunifu wako, unda nafasi zako za kuwafikia vijana kwa njia ambazo zitajitambulisha na mahitaji ya wanafunzi na baadaye utumie ujumbe wa Injili katika mahitaji yao. Ili uweze kujua jinsi ya kufanya hivyo tumia kifaa cha *Athari ya Sumaku* katika kurasa za kutayarisha mpango. Zitakusaidia kuunda mpango wako ili uweze kuwasilisha ujumbe wa Kristo kwa njia bunifu na iliyo na matokeo.

5. **Ni vyema kufanya mikutano ya kuwafikia wengine ndani ya kanisa au mahali pasipopendelea upande wowote?**

Sheria ni kwamba, ufanye chochote kiwezekanacho ili uweze kutoa vizuizi vinavyozuia wanafunzi kumjua Kristo. Ukiwa na mambo hayo katika akili yako utahitaji kuangalia mahali pa kukutana na nafasi uliyonayo ya uchaguzi katika jumuiya yako, baadaye waweza kuamua ni mahali gani patakuwa rahisi kwa wanafunzi wasio Wakristo kuja. Gharama, mpango, juhudi, urefu na utambuzi wa mahali hapo kulingana na jumuiya yote yatachangia katika uamuzi wako. Njia moja ya kuamua ni kuwachunguza vijana wako, na wanafunzi walio katika vyuo ili uweze kujua ni mambo gani yanayowavutia.